

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

CKRC

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

MARAKWET EAST CONSTITUENCY, HELD

AT CHESONGOH PRIMARY SCHOOL

ON

JULY 3RD 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS HELD AT CHESONGOH PRIMARY SCHOOL ON 02/07/02

COMMISSIONERS PRESENT

1. Com. Dr.Githu Muigai
2. Com. Ibrahim Lethome
3. Com. Bishop N. Kariuki

SECRETARIAT STAFF PRESENT

1. Mr. George Nakholi - Programm Officer
2. Mr. Wambua Kagangwe - Assistant Programm Officer
3. Mary Babu - Verbatim Recorder
4. Solomon Kibet - District Coordinator

The meeting was called to order at 10.20 a.m with Com. Ibrahim Lethome chairing.

Solomon Kibet: People of Chesongo kabla tunangoja watu wakuje tutafungua kikao kwa maombi. Nafikiri nitamuomba mwalimu Langat atuongoze kwa maombi. Mwalimu Jacob Langat.

Jacob Langat: Tuombe pamoja kwa jina la Baba, la Mwana na Roho mtakatifu. Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe ufalme wako ufike, utakalo lifanyike duniani kama mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kila siku, utusamehe makosa

yetu kama tunavyo wasamehe na sisi wale waliotukosea. usitutie katika kishawishi, lakini tuokoe maovoni Mungu mwenyezi tunakuja mbele yako saa na wakati kama huu, tunasema asante kwa nafasi kama hii, tunasema asante kwa zawadi ya hawa Commissioners, ambao umetuletea hapa kusudi hasa ya urekebishaji wa Katiba. Tunaomba pia kwa ajili ya wale ambao hawajafika, Mungu mwenyezi waongoze wafike hapa salama. Tunaomba pia kwa ajili ya yale ambayo tutaongea, Mungu mwenyezi tunaweka mikononi mwako, tukiamini yote utatutendea. Pia tunaomba kwa ajili ya urekebishanji huu wa Katiba Mungu mwenyezi ili uweze kutufaidi sisi kama waKenya, uweze kutuletea amani katika eneo hili la Kerio Valley. Tunaomba hayo yote kwa njia ya Kristo bwana wetu. Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho mtakatifu. Amen.

Solomon Kibet: Asante kwa kutuongoza kwa maombi, ningependa kuwajulisha kwa CCc members, kuna John Kipyatich, na kuna Anthony Kiplagat. Commissioners ambao wako hapa leo, tunaye Commissioner Ibrahim Lethome, tunaye Commissioner Dr. Githu Muigai, na tunaye Commissioner Bishop B.N. Kariuki. Commissioners mtaturuhusu kwa sababu watu bado wanakuja polepole, wanatoka huko juu kunaitwa Lagam, wanateremka pole pole saa hii bado wanasema ni asubuhi lakini watafika tu. Nitamuita Girwagin Chief, ili ampishe Commissioner Ibrahim Lethome anzishe mkutano. Girwagin

Lawrence Girwagin: Ma-Commissioners ambao wako hapa waKenya ambao waliandamana pamoja tunasema pole kwa safari ndefu na hata kwa vile tulijulisha juzi watu kwamba tutakuwa na mkutano leo mkubwa sana. Tunaomba tu kwa vile Coordinator alisema watu wanatoka kule juu mlimani na wakati tunaendelea, tunaendelea tu na kazi yetu ili wale wengine watatukuta kama tunaendelea. Tunasema karibu, karibuni hapa Chesongoch kwa niamba ya wananchi ya Mkutwa, wa Tot mzima, tunasema karibuni, asante sana.

Com. Ibrahim Lethome: Asante sana Bwana Chief, Lawrence

Chief Lawrence: Kwa jina naitwa Lawrence, kuko ma Chief watatu hapa.

Com.Ibrahim: Basi wewe umezungumza kwa niamba ya wengine watatu. Kwanza watu wa Chesongoch hamjambo!

Audience: Hatujambo!

Com. Ibrahim Lethome: Asanteni. Coordinator can the children also come and take seats at the back or so lets not discriminate against them let them come, the youth. Kwanza tunamshukuru mwenyezi Mungu ambaye ametufikisha hapa kwa usalama na kutuwezesha kuwa na mkutano huu, na kama mnavyo jua leo sio siku yetu kama Commissioners kuzungumza, wala sio siku ya Chief ya kuzungumza au mtu mwingine yeyote, leo ni siku yenu ya wananchi kuzungumza na kutoa maoni yao kuhusu marekebisho ya Katiba. Ni siku ya kihistoria kwa sababu ni kwa mara ya kwanza katika taifa letu tumepata nafasi kama wananchi kusema tunataka tutawaliwe vipi? Tunataka sheria na siku za usoni za nchi hii ziwe vipi. Ni siku yenu ya kuzungumza na ninajua mmejitarisha vilivyo kuweza kutoa maoni yenu.

Ningependa tu kwanza kuwajulisha nafikiri mmejulishwa ma-Commissioners ambao tuko nao hapa, Commissioner Dr. Githu Muigai, na Commissioner Bishop Bernard Njoroge ambaye ndio kiongozi wa msafara huu wetu wote. Yale makundi yote yako huku Marakwet yeye ndio kiongozi wetu. Ningependa tu kuwajulisha baadhi ya utaratibu ambao tutakaofuata katika mkutano huu wetu wa leo kwa sababu panapo watu wengi lazima pawe na utaratibu. Hata ikiwa ni mchezo wa mpira kuna utaratibu wakt na kuna sheria zake, ili tuweze kufaidika na ule wakati.

Kwa hivyo bila kupoteza wakati nitawapeleka juu ya huo utaratibu na pia ni vizuri pia niwajulishe ma-officer ambao tumekunja nao kutoka katika idara yetu, wanaosimamia kazi hii. Tunaye Officer pale ambaye ni Programm Officer anaitwa George Nakholi, yeye ndie msimamizi wa idara ya kazi yetu ya leo. Kule nyuma tunaye Mary, Mary unaweza kuonyesha mkono Mary.

Mary kazi yake ni kunasa ndio unaona amekaa huko mbali kwa sababu anataka kukaa karibu na kipaza sauti kuweza kunasa sauti zenu kwa kupitia kile chombo cha kunasia mazungumzo. Kisha tunaye kijana ambaye anaitwa Wambua, yeye kazi yake ni kusajili kwa maandishi yale yote ambayo mtakayo zungumza kwa sababu hatutaki maoni yoyote yapotee. Kwa hivyo hao ndio tutakao aidiana na wao tutashirikiana na wao leo.

Utaratibu wa kwanza katika kutoa maoni, kuna namna mbili ya kutoa maoni: namna ya kwanza ni kuwa na maandishi Memorandum. Ikiwa una maandishi ambayo ungependa kutupatia, basi nitakupatia dakika tano. Ikiwa unataka kuzungumza upitie katika hiyo Memorandum bila kuisoma yote, Utaangaza highlights, yale ambayo ni ya muhimu kwa hizo dakika tano halafu utatukabidhi hiyo Memorandum na ikiwa Commissioners wana swali lolote wataweza kukuuliza kutaka ufafanuzi clarification kutoka kwa hiyo Memorandum yako. Kwa hivyo ukiwa na maandishi nitakupa ndakika tano ikiwa hutaki kuzungumza unataka kutukabidhi tu hiyo memorandum yako, utakunja useme jina lako kisha useme mimi nina memorandum ambayo ni maandishi nanitawakabidhi utamkabidhi bwana Nagholi.

Namna ya pili ni kuwa mtu ambaye hana memorandum oral presentation, unataka tu kuja kuzungumza na kutoa maoni yako, nitakupatia dakika kumi uje hapa, useme jina lako kisha ueleze. Lakini katika kule kueleza dakika kumi ni chache sana, tulipoanza mpaka sasa ndakika kumi zimeisha na hatujazungumza mambo mengi. Kwa hivyo tungependa upendekeze to recommend. Unajua kuna problem ya insecurity, usianze kutuambia kuanzia mwaka fulani hadi sasa kuna problem kadha, watu kadha wamekufa, barabara ni mbaya na nini, pendekeza unataka nini? Kwa sababau sasa tunaangalia mbele. Tunajua hayo ni matatizo ambayo tuko nayo, tunataka nini sasa, ili tuwe na mabadiliko mazuri. So you recommend uki-recommend utafaidika na hizo ndakika zako kumi, ili kila mmoja aweze kupata nafasi ya kuzungumza. Bwana Coordinator ametwambia watu bado wanateremka mlimamo kwa hivyo baadaye najua hii nafasi itakuwa hata haitoshi watu watakuwa ni wengi sana.

Kisha upande wa lugha una uhuru wa kutumia lugha ambayo wewe mwenyewe unataka ikiwa unataka kuzungumza ki-Marakwet, zungumza tayari bwana Coordinator ametutayarishia mtu wa kufasiri interpreter. Yule kijana aliye na kofia nyekundu kazi yake ni ku-interpret kwa hivyo zungumza ki-Marakwet, ki-kalenjin, ki-pokot, kuzungumza kiingereza, kiswahili

una uhuru wa kuzungumza hizo lugha zote. Kisha lazima tuheshimu maoni ya watu wengine, mtu akija hapa kuzungumza na kutoa maoni yake ikiwa yale maoni haya kukupendeza wewe tunakwambia hayo ni maoni yake, tuyaheshimu tumuachie amalize bila kupiga kelele wala kumzolea. Wewe nafasi yako ikinja, ukitaka kuja kumpinga au kupinga maoni yake mpinge, lakini hatutaki kusikia makelele huko nitatoa red card. Unajua referee anvyotoa red card, ukicheza vibaya nitatoa red card hapa nikwambie sasa umekeuka mipaka,hiyo tumekubaliana, tuheshimu maoni ya wengine.

Halafu mwisho kabisa hatutaki mtu akose kutoa maoni kwa sababu anaogopa, anaona nikizungumza habari ya Chief na Chief yuko hapa, Chief atatuma askari wake waje wanishike au nikizungumza habari ya ofisi ya DO nitafuatwa, au nikingumza habari ya polisi kuwa polisi wanaumiza wananchi, wanawanyanyasa wananchi nitashikwa. Sheria imewekwa na serikali yetu au na mbunge letu kuwa, kila mkenya ana uhuru wa kusema vile anavyotaka, na hawezi kufuatwa kwa sababu ya kutoa maoni yake. Kwa hivyo utoe maoni yako bila uoga.

Jambo moja tu, hiki siyo kikao cha kisiasa, mambo ya siasa yatakunja baadaye utafanya siasa katika kikao cha siasa. Hatutaki kusikia matusi unamtukana mtu yeyote au unamtanja mtu yeyote kwa ubaya ama nini, hatutaki mtu atanjwe kwa majina, zungumza habari ya cheyo, lakini usisungumze habari ya mtu. Kwa hivyo hatutaki matusi wala kuingiliana, hatukuja hapa kutukanana, tumekunja hapa kutoa maoni yetu kuhusu sheria tunavyotaka. Lakini una uhuru wa kusema unavyotaka hata kuhusu tume hii ikiwa unasikia jambo fulani linakukera kuhusu tume na unataka hayo maoni tuyapate, toa hayo maoni katika zile dakika nitakazokupa. Na kama nilivyo waambia kuna kitabu pale cha ki-historia ambacho utasajili jina lako, na kuweka anwani yako na sahihi yako, itakuwa ni kumbukumbu ya ki-historia kuwa ulishiriki katika kutengeneza Katiba mpya. Sasa bila kupoteza wakati tutaanza, na mtu wa kwanza ambaye atakaye tuanzia ni Jacob Langat.

Jacob Langat: My names are Jacob K. Langat, I am presenting this document on behalf of Kerio Valley Group. My (inaudible) to present is Preamble.

Now our Constitution requires a Preamble na kwa hii Preamble sisi watu wa Marakwet, sababu we can (inaudible) in cattle life we need security hiyo ni ya kwanza, Because here in Kerio Valley, we are really forgotten by the Government in terms of security we are all the time (inaudible) by the Pokots while the Government is actually watching from the fence, we are really suffering we are marginalized in terms of development, hakuna justice, and the role of the g Government, to set some some aid forces bases along the Kerio River,

Interjection Com. Njoroge: Mr. Langat face this way,(inaudible) do not face the radio, face us two very simple once please,

Mr.Lagat: Ok, so tunataka serikali waanzishe police stations in Kerio River ili wazuie wa-pokot wasivamie wa-marakwet.

Ya pili tunataka free education kutoka nursery mpaka University, tunataka health services. hapa Kerio Valley hatuna health

centres kutoka kwa serikali iko tu Private health centers, sasa sisi tunataka health centres kutoka kwa serikali. Tunataka free and fair elections ifanyiwe hapa kama kuna general election. Tunataka protection of our properties mali yetu ikuwe protected by the Government, Government ichukuwe hiyo kama responsibility yake ku-protect our properties. Tunataka liberty tuwe na freedom ya kufanya yoyote. Tunataka preservation of our environment and natural resources. Sisi tuko na forests na saa hizi imevamiwa sana. Karibuni tutakosa maji sasa tunataka Serikali ichukwe hii kama jukumu kuhakikisha ya kwamba hii forest imekuwa conserved.

Tunataka kuna promotion of some cultural values. Hapa tuko na cultural values zile ziko muhimu sana, kama mambo ya land disputes ikuwe settled na council of elders, and these people should be empowered to ensure that the land disputes are reduced. Tunataka kuongozwa na sheria.

Ya tatu ni tunataka common philosophy hatutaki yule mtu kama President mmoja akija, anakuja na philosophy yake sisi kama waKenya tunataka philosophy moja.

Na ya tatu kuna hii mambo circumcision tunataka mambo ya circumcision isikuwe kitu kama lazima. Wacha circumcision ikuwe optional mtu akitaka kuwa circumcised anachagua, kama anafika miaka kumi na tano.

Interjection: Com. Githu: Male or female or both?

Langat: Both, kwa sababu siwezi sema ati hata hii watu wavulana wachaguwe wako na freedom ya kuchagua, mtu akitaka kukaa bila circumcised ok akae. Kuna hii mambo ya shamba boundary yote ya Pokot iko mbele ya Kerio river, inaitwa Arapen. Sasa hawa Pokot waheshimu boundary yetu. Hawa Pokot wanakuja kunyanganya sisi nyasi yetu sisi watu wamarakwet tunakataa, tunataka nyasi yetu tutumie wenyewe. Tunataka tena hii property inatoka kwa forest yetu Wamarakwet wenyewe watumie, isiende kwa serikali. Kwa vile wenzangu watafanya ile nimefanya hapa nimeimalizia.

Com. Ibrahim Lethome: Asanti sana Langat any question Commissioners? Ok. Asanti just hand over and register. Peter Cheboi, hayuko. Ok. Cheboi, again I remind you if you have a memorandum just highlight do not read the memorandum, we shall read every word. Just sit down, it might be better for the recording.

Peter Cheboi: Ok. I am going to read the directives

Com. Ibrahim Lethome: just sit down.

Peter Cheboi: My names are Peter Cheboi. I am presenting this document, and these area collection of views by people of Kerio Valley. So I have been given the responsibility to read directive principles of state policy. These are what the people

collected. So directive Principles of State policy statements are required in the Constitution. We are told that there are no directive principles in the current Constitution which is guiding us Kenyans now. We want democratic principles to be included in the new Constitution, and this includes the limits of the President's powers to enhance democracy. We want the limits of the President's powers, so that the President should not go past the limits which are required by the democracy in our country.

Secondly, we want transparency and accountability of the governance. There should be transparency which must be entrenched in the Constitution, also accountability, because we know that in this country the issue of transparency and accountability is not there. Also we want equity of all citizens in land. We are told that some people have vast land and others do not have land. Some people live below poverty line because of land problems, therefore we want the Constitution to enhance this issue of land equity. Also respects of fundamental rights and freedom, there is no respect in the current Constitution of fundamental rights though they are written, they are not practiced at all.

Also we want proper establishment of Institutions and their management. The institutions that are all over the country they have to be properly managed. Also establish the rule of law without fear and favor. We want this new Constitution, the Constitution which will guide us in the nearby future to have a rule of law which enables people to rule without fear and favor. Also we have values to be reflected in the Constitution and these values include morals for leaders. Our leaders should have morals lazima wawe na sifa nzuri, wasiwe watu wenye wako na criminal record. Also we want in what we call patriotism for all citizens. Kenyan citizens must be patriotic in order to enhance the development of the country and also to protect the image of the country.

Also total responsibility we want the Constitution to entrench the issue of responsibility in the current Constitution, so that the leaders must be responsible in all the endeavors in the country. Also justice in Kenya: we do not have justice and we want justice to be exercised everywhere in the country. Finally promotion and protection of traditional cultures and their variety. For example we have those tradition culture that have to be enshrined in the Constitution. For example, traditional dancers, we have some traditional dancers which may provide or which may enhance the country to earn foreign exchange if tourists came and then these people are entertained by these people, then they will earn the country foreign exchange, but we see that these traditional or various traditional.....

Interjection Com Lethome: you have made your recommendations give us something else.

Lagnat: I think I am through with what I have written

Com.Lethome: Ok. Present you will present your memorandum there. Can I have the microphone? Nitarudia tena sababu ya kutumia hiki chombo, siyo usikike tu, ni kwa sababu ya ku-record, it is more for the recording purpose than for either being audible or inaudible. Can I have the children present? Because they might be going back to school. Watoto wa skuli ni nani anazungumza kwa niamba yenu? Au mmekuja kusikiza tu? Mmekuja kusikiza ama mnataka kutoa maoni. Haya yule mwenye kuzungumza aje hapa mbele. Nani anazungumza? Who is speaking on your behalf? Kujeni wale wanazungumza. You are

wasting time watoto. Ok. Can we have Almond Kuto? I want to release you because you might want to go back to school, so come over. Mwalimu wao yuko hapa? Mwalimu how come your kids are not obeying? so you are training them, these are going to be the leaders tomorrow, the leaders of today. Keti hapa toa maoni yako halafu useme jina lako.

Chemutai Tekla: My names are Chemtaki Tekla I am a pupil from Chesongoi Primary school, and I am a candidate.

Interjection Com Lethome: Class 8, how old are you Chemtai?

Chemtai: Yes 14 years. As pupils, we want free education and even more to participate in games and sports. In addition to that we also want National schools to be built in our districts not only in Nairobi Province. Also we want to know the subjects which have been reduced may be even the next time it may be reduced to be last year it was 8 and it was reduced to be 5. We do not know, may be the next year it will be 4, who knows, we want a permanece subjects, if it is 5 to be 5, if it is 8 to be 8. That is all.

Abel Kipchumba: My name is.

Com. Ibrahim Lethome: Wewe kijana Msichana alizungumza anasikika vizuri lakini wewe husikiki. Zungumza kwa nguvu zaidi. Songa mbele kidogo.

Abel Kipchuba: My name is Abel Kipchumba

Interjection Com Lethome: How old are you?

Abel Kipchumba: 15 years.

Interjection Com Lethome: 15, which class are you? Std 8 very good haya Kipchumba zungumza.

Abel Kipchuba. We as candidates hapo zamani mbeleni tulikuwa na mchezo, lakini saa hizi michezo ilikuwa inatusaidia wakati wa zamani kwa miili yetu kwa kupata afya. Lakini wakati wa sasa hatuna michezo na tunataka michezo iwe kutoka saa hizi indelee ndio tupate afya katika mili yetu. Na tunataka amani kama sisi wanafunzi kwa vile tunasumbuliwa kila wakati tukiwa darasa tunasikia ngurumo za bunduki zikilia, tunazitotoroka, kufika tunawacha mashule zetu ziharibike huku chini, tunaenda mpaka huko milimani kujenga mashule zingine ambazo tunateseka kabisa huko. Nyoka ziko, tunasomea kwa mamawe, miti, na tunataka amani irejee ndio tusomee mashule zetu ambazo tulikuweco. Asante.

Com Lethome: Asante sana nenda ukajiandikishe pale, lakini uwangonjee wenzako pale, unajua mkiondoka, ondoka hawa wamebaki wataanza kutetemeka. Kaa hapo uwangonjee wenzako hapo. Hebu tumsikize huyu mzee mwingine.

Elias Koskei: Kwa majina naitwa Elias Koskei.

Interjection Com Lethome: Koskei unasoma darasa la ngapi?

Elias: Darasa la nane.

Com Lethome: Hebu twambie umri wako Koskei.

Elias: 14 years.

Com. Lethome: Songa hapa hivi ili Commissioner wengine wakuone vizuri. Miaka kumi na tano?

Elias: nne, ndio

Com. Lethome: Kumi na nne, ndio. Tunakutakia ufanisi katika mtihani toa maoni yako.

Elias: Sisi kama wana wa Chesongoi na wananchi wengine tuna haki ya kuishi. Na kama tuna haki ya kuishi, kweli tunasumbuliwa na wapokot. Jee kama serikali wanafanya kazi gani? Tunaonelea ni kweli kuwa tunataka tuchungwe na serikali yetu ya Kenya, na serikali hii, wa hakikishe kuwa hakuna raia yeyote ambaye ako na bunduki lolote:

Interjection Com. Lethome. Kuna bunduki huko? Wanyanganywe bunduki zote?

Elias: Ndio kama Wapokot,

Interjection Com Lethome: Na Wamarakwet wale wako na bunduki?

Elias: Hawana, laughter from the audience. Na ya pili, tunataka katika kila wilaya ijengwe National schools na hospitali. Asanti, that is all.

Com. Lethome: Hebu tumsikie mwingine, sema jina lako?

Monicah Bowen: Kwa majina naitwa Monica Bowen.

Interjection Com Lethome: Monicah unasoma darasa la gapi?

Monicah: Darasa nane.

Interjection Com. Lethome: Haya na una umri gani?

Monicah: 15 years.

Com. Lethome: Toa maoni yako Monica.

Monicah: Kwa mimi kama mwanafunzi sisi hapa kwa Kerio Valley tumetaabika sana kwa security au kwa kimasomo . Kila siku tunatoka huko mbali, huko escarpment, sasa tukifika shule hatupati preps za asubuhi.

Interjection Com Lethome: Kwa nini?

Monicah: kwa sababu tungeishi karibu na shule, sasa tunafukuzwa na pokot tukaenda huko escarpment sasa shule imekuwa bali sana.

Interjection Com. Lethome: Unataka sasa serikali ifanye nini kuzuia pokot?

Monicah: Watupatie maaskari wengi. Na shida ya pili, tunataka Serikali itupatie chakula, enough food, ili tuweze tusome vizuri na tukule. Kwa sababu usipokuwa ana afya hutasoma vizuri kwa sababu ya njaa. Sasa tunaomba Serikali watujengee hata ma hospitali kwa sababu kila siku wanafunzi wanakuwa wagonjwa na hospitali sio karibu. Sasa tuko na few health centres na ni Private. Sasa tunataka Serikali watujengee ili tuweze kutibiwa magonjwa. Asante.

Com. Lethome: Sasa wale walianza kuzungumza wanaweza kujiandikisha.Wacha tubaki na hawa watatu basi. Sema jina lako.

Beatrice Komen: Kwa majina naitwa Beatrice Komen.

Interjection Com. Lethome: Beatrice unasoma darasa la gapi?

Beatrice: Nane.

Interjection Com. Lethome: Una umri gani?

Beatrice: Kumi na nne.

Com. Lethome: Haya zungumza.

Beatrice: Kama sisi wanafunzi tunataka simu ikuje shuleni mwetu.

Com. Lethome: Haya vizuri una nyingine? Ni hiyo tu? Haya ita mwenzako.

Beatrice: Asante:

Com. Lethome: Sema jina na useme maoni yako.

Beatrice Kitum: Kwa majina naitwa Beatrice Kitum.

Interjection Com Lethome: Beatrice nani?

Beatrice: Kitum.

Com. Lethome: Kitum unasoma darasa la ngapi?

Beatrice: Ninasoma darasa la nane.

Com. Lethome: Una umri gani?

Beatrice: Kumi na tatu.

Com. Lethome: Toa maoni yako.

Beatrice: Sisi kama wanafunzi tunataka Serikali wanapopeana vitabu viweze kufika upande huu. Hata tunataka tuendeleze michezo. Asanti.

Com.Lethome: Inginge, haya mngojee mwenzako usimuache peke yake. Sema jina lako.

Miriam Biwot: Kwa majina naitwa Miriam Biwot.

Com. Lethome: Miriam unasoma darasa la ngapi?

Miriam: Darasa la nane.

Com Lethome: Una umri gani?

Miriam: Kumi na tano.

Com. Lethome: Haya toa maoni yako.

Miriam: Kwa maoni yangu kama wanafunzi tunataka tusaidiwe na Serikali na school uniform free of charge. Kwa sababu ya shida balibali ambazo tunazo.

Com.Lethome: Haya kitu kingine:

Miriam: Ni hayo tu.

Com.Lethome: Ngonja kidogo kuna swali

Com. Bishop Njoroge: Ningetaka kuuliza kwa nini hamchezi? Kwa nini? Ni kwa vile waalimu hawapatii michezo au ni kwa nini?

Miriam. Kwa security.

Com. Lethome: Semeni kwa mic.

Miriam. Kwa sababu ilipitishwa na Serikali kwamba hakuna activity fees, activity funds.

Com. Bishop Njoroge: Activity?

Miriam: Ati hakuna pesa.

Com. Bishop Njoroge: Lakini kucheza si ni kukimbia tu kwani Serikali ni lazima iwasaidie kucheza kama vile mwanafunzi mwingine alisema.

Miriam: Hakuna usalama.

Com. Lethome: Asanteni wanafunzi. Mmeingia katika historia katika kumbukumbu za historia kuwa mmeshiriki katika kutengeneza Katiba mpya. Watoto wenu na wajukuu wenu wakuwa wakisema hawa walitoa maoni yao katika Katiba mpya. Haya tunaendelea Almond Kuto, karibu David Kada we have tu move fast na David akae tayari. If it is a memorandum you highlight. Say your name and begin giving views.

Almond K.Kuto: My name is Almond K. Kuto. I am going to present my views on Constitutional Supremacy. We expect to have two chambers of Parliament, the lower and the upper house. The lower house should have 75% and the upper house should have 90% of majority votes. Parliament should have limited power to amend the Constitution, because the citizens are the people who are supposed to make the laws, like right now we are presenting our views. We want parts of the Constitution to be beyond the ammedingi power of Parliament are as follows:

Land issues, scaling of Parliamentarian salaries and allowance should be done by an executive body not the Parliamentarians themselves.

Electoral process and voting system the Public through referendams should be involved in amending Constitutional parts, those which are affecting the Members of Parliament and their benefits visions.

Next is Citizenship, the details contained in the National Identity Card are not enough. We expect that a person should be registered in his local authority. Like the county council should be added in the identity card. That a person should be registered in his local authority so that, if he has a problem if he does a mistake, he should be known upto the locality.

Acquisition of Kenyan Citizenship: if a father, mother, both parents are Kenyan citizens, he should acquire Kenyan citizenship. A person who has lived in Kenya for 10 years, he is required to be having a good reputation and would acquire Kenyan citizenship. Spouses of Kenyans regardless of gender should be entitled to automatic citizenship. Children born of Kenyan parent's regardless of parents gender, should be entitled to automatic Kenyan citizenship.

Rights and obligations of Kenyan citizens: Kenyan citizen should get right to life, right to own property anywhere in the country no matter where a person comes from right to education, health facilities, voting and at the attainment of 18 years and above right to security and protection of property right to shelter clothing, right to employment opportunities rights to access to social amenities, right to access to clean water, right to food security, right to religion.

Obligations of Kenyan citizens. Kenyans should abide by the law and respect the Constitution. They should be patriotic economically, politically, socially, culturally, traditionally and spiritually to their country. Respect for people's life and

properties.

Towards citizenship: towards citizenship under normal circumstances for security purposes economic protection political stability, the Constitution should not allow for dual citizenship, it should not be there. Documents that Kenyans should carry as evidence for citizenship that is the National Identity Card and the Passport. Thank you.

Com. Lethome. Thank you Almond, David Kanda. Na Patrick Komen akae tayari.

David Kanda: Mimi ni David Kanda nataka tu kutoa maoni yangu. Yangu sana naongea juu ya barabara. Tunataka sisi kama Wamarakwet tufanyiwe haki zetu. Kwa sababu tangu tulipojinyakulia uhuru, mawaziri wetu waliimba mambo ya barabara na sana sana, Serikali wanajibu ya kwamba wametosheka, na kumbe kutosheka kwao ni kudanganya. So tunaona kama tumepata hasara nyingi. Unaona tukikuja kama upande wa Keiyo, tunazungukwa na lami, imewekwa lami imezunguka nyingine imefika Keiyo, nyingine imeenda upande wa West Pokot, na sisi kweli hapa kwetu ni fupi. Tunataka tu Serikali watufanyie mambo ya barabara waweke rami. Ili mawasiriano iwe rahisi, kwa sababu tunapata shida kama mambo ya security, watu wote wanauawa hapa na tunapiga simu na Serikali kweli wanakuja kama tumekaa kama siku tatu.

Na nyingine kweli ni kwamba serikali wanatupatia pesa ya mambo ya makadirio na kweli tunapatiwa kama milioni tano zinakuja mpaka headquarter state ya Kapsowar. Kweli huko kuna watu tunaita syndicate sijui ndio mafia, wanakuja kufanyia record zao na sisi kweli hatupati hivo vitu. Tunataka pia Serikali, hao watu wawekwe ndani isije ya kwamba wafanye ati wanapigwa transfer, unapiga transfer mtu mwizi kutoka marakwet aende Kajiado, si ataenda kukuwa mwizi huko tena? Mtu awekwe ndani hapo, hapo.

Kweli Serikali yetu tukufu wanajua ya kwamba tuko na shinda, naona hata msafara wa raisi kweli wanakuja pande huu wanapitia helicopter kwa sababu wanajua kweli barabara ni mbaya. Na hata juzi tulipata haya mambo ya ile massacre tulipata hapa Mrukutwa. So hata Serikali hawakutujali, wali-fill tu helicopter na kupeleka hiyo meeting yao huko chini, msituni na sisi tunaumia upande huu kwa sababu wanajua barabara ni mbaya. So sisi wamarakwet tunalia mambo ya barabara. Hata saa hizi hata hatuna matatu, hatuna mabasi tunakuja kulala hapa halafu tunakanyaga about 50 kilometers halafu tupate magari huko juu.

So tunataka hiyo ni yetu, na pia mambo ya Parliament nataka kuongea juu ya hayo. President hizo power zake ziwekwe chini kwa sababu he cannot dissolve Parliament by himself, kwa uwezo wake mwenyewe. Hayo mambo ya Parliament wafanye ya kwamba, Bunge isajili ya kwamba wanafunga Parliament adjourn, kua siyo jukumu la Rais kusema Parliament ifungwe mpaka wakati fulani. Hata kweli nataka kusema haya mambo ya Commissioners yasije yakapewa mda, mpaka mwaka ujao, iwekwe kama mwaka huu iishe halafu next time tupate Katiba mpya. So ninataka tu kusema asante na tunalilia barabara yetu.

Com. Lethome: Asante David, Patrick Komen, na John Komen akae tayari, John yuko karibu, ni Yomen ama Komen,

Audience: Komen.

Com. Lethome: Haya mfuatane vizuri

Patrick Komen: My names are Patrick Komen na I am presenting basic rights. Our Constitutional, provisions for fundamental rights are not adequate, other rights to be entrenched in the Constitution. Traditional medicine surgery, the government should sponsor the people during the surgery and medication for hygiene requirements. Conservation for herbal medicines. Death cases and land cases be dealt with by the community. Let the people have alternative ways of resolving problems or disputes. Matters should be dealt with by the court of law instead of punishing the clan. Village or community at large by the people, who have lost their relative. A criminal should be punished alone Death penalty should be abolished and life sentence be guaranteed. Its against God's commandment to kill. Its not a lasting solution to be a problem. Government to improve the living standard of Kenyans. Also make Kenya as a nation attain economically adjustment and industrial youth centres. The Government should have its responsibility of ensuring that all Kenyans enjoy the basic rights.

Those with illegal fire arms to be disarmed by the Government, and recruitment of enough security officers.

Health Care: Each Kenyan should have access to quality health care.

Water: There should be plenty of clean drinking water for every Kenyan.

Education: Educations should be free and compulsory to every Kenyan citizen from nursery to form four, and access to loans and bursaries in the Universities and colleges. Learning resources should be freely provided by the Government, teachers should be employed particularly by the Government and distributed fairly.

Food security: The Government should provide food security. The Government should provide certified seeds to the farmers. Land security to be provided. Strategic food reserves or stores to be built by the Government.

Employment: The Government should create employment opportunities and ensure every Kenyan is employed formally or informally. Employment should be by merit. Nepotism, tribalism, clanism, should be avoided. Corruption on employment should be also avoided. Kenyans have the right to access of information regarding their state. Right to information should be funded by the Government, for example appointment of the Commission. The Constitution guarantee trade union representation, whether private or public for the people to express their problems. Other basic needs of Kenyans that the Constitution should guarantee, good infrastructure e.g. roads, communication equipment like telephone, rural electrification, and land ownership. Thank you very much.

Com. Lethome: Thank you very much Patrick. Can I have John Komen now.

John Komen: Mimi ni John Komen, natoa maoni kwa niaba ya watu wa Kerio Valley on political parties. Political parties should play other roles in aid of development. These roles are:

- a) Ensure that the distribution of national resources is fairly done. Each political party should ensure that there is accountability and transparency in the National budget.
- b) All political parties should participate in development of the nation. They have the duty to educate the citizens on their electoral rights and processes.
- c) All political parties should focus on gender sensitivity. All political parties should focus and advocate for security of the citizens. The Constitution should regulate the formation, management and conduct of political parties so that, each political party should focus on all intended regulations.
- d) The limit of political parties should be 3. In Kenya we should have at maximum 3 political parties, in order to avoid tribalism, to allow national presentation. Political parties should depend on themselves by looking for donors from foreign countries and even within, instead of using public funds.
- e) Terms and conditions to be imposed in financing political parties, that means all political parties should be treated equally, if they are three. There must be a limit on the amount of money to spend during campaign rallies. Campaign procedures should be harmonized to all political parties. The political parties should be treated equally, there should be no favouritism for any political party.
- f) **Relationships of state and political parties.** They should be inter-independent on one another, because all political or all development matters are discussed by the state and political parties. They should have a common link because all the matters relating to the management of the Government are discussed in the Parliament. They should have common relations in terms of dealing with public finance. All should strive and see to it that all National resources are fairly distributed. With that thank you.

Com Lethome: Thank you very much John Bowen. Bowen Suter yuko, and Peter Suter wafuatane hivyo.

Bowen: *Omwochini bichu bo commission nemji kile, kongoi amu kabate ng'alek ab markweta.*

Translator: Asanti kwa kufika kusikiza maoni yetu.

Bowen: *Ko kwotar kirikimi yu nye bo tai ko ng'alek bo mbarenik.*

Translator: Ya kwanza ni kuhusu mashamba.

Interjection Com. Lethome: Shikia hapa ndio ifanye, rudia tena mwalimu.

Translator: Ya kwanza ni kuhusu mashamba.

Bowen: *Ng'alek bo mbaretin ko koroni ko kichoran boik kong'eten nyuma ago inget clan.*

Translator: Mashamba yalipochorwa na wazee hapo mbeleni na wao ndio wanamudu akili kuhusu mashamba.

Bowen: *kemoche any kimwochini wakati ya katiba kimoche boik cho kisir cho koip ng'alek ab mbarenik*

Translator: Tunaomba kuwe na kamati ya wazee katika wilaya ili watatue mambo ya mashamba.

Bowen: *Amu ki kityo kaseret bik amun ki mi siasa, ago mi nee, u warkach ago bicho kosere bik cho muche kosere bik en yu.*

Translator: Kwa sababu kumekuwa na wizi sana sana kupitia upande wa wanasiasa, ambao wao ni matajari, na hunyanyasa walio wanyonge.

Bowen: *Ko ng'olio nebo somok, komwochi serkali kirip kertit nguni nenyon, amun kertit komong'ering chomenye age tugul mi sakitianda, mi kumita, mi ker*

Translator: Neno lingine la tatu, ni kuhusu ulinzi wa msitu, twataka Serikali iwajibike katika ulinzi wa msitu, kwa sababu misitu hutupatia dawa, asali, na maji.

Bowen: *Ko nyo miten ko kongoi manee ne muchache chebo boit*

Translator: Nasema asante kwa sababu hiyo nimesema kwa niaba ya wazee wenzangu.

Bowen: *Kongoi missing, kainenyun kekuren Kiboen Suter Ramchin.*

Translator: Naitwa Kibowen Suter Ramchin.

Com Lethome: Peter Suter.

Peter Suter: My name is Peter Suter, I want to present part of the executive. Provincial Administration. The Provincial Administration, the duties and responsibilities, job description, must be clearly stated by the Constitution, in a situation where people or Provincial Administrators, promotion should be continuous basing on the confidence of the Provincial Administrators that is Assistant Chiefs, Assistant Chiefs to Provincial Commissioners, that is now from Chiefs to even DO, from assistant chief to DC because if he has his papers.

The roles of Provincial Administrators: To ensure security of their citizens, present the needs of the people to the Central government, to be in charge of the civil servant in his place if he is assistant chief, or chief; maintenance of order, protection of environment and the natural resources, settling land disputes between various warring groups, initiating development projects in their respective areas, implementing Government policies in their respective areas; I would like to recommend, because the assistant chief or chief is in charge of everything in his sublocation, or location, he should be given more salaries because assistant chief or Chief is having a very little salary, and every minute he/she is to be called to assist wananchi. So that is what I have and another recommendation that I wanted to put in is that, interference from politicians yaani wanasiasa, pengine ningependa wanasiasa wasiingilie administrators kwa kazi yao. Wanafanya kazi yao iwe ngumu sana. Hawa wanasiasa wafanyana kazi yao laini yao, mambo ya Administrators wafanye kazi yao ile kazi iende vizuri, kwa hivyo ni hayo tu, thank you.

Com. Lethome: Asanti sana, bwana Peter Lawrence Suter,

Lawrence Suter: My name is Lawrence Suter, mimi nataka tu kuongea ambayo nitachangia kidogo, ni kuhusu station kwa employ watu. Hapa Valley tuko na shida sana, kwa sababu wakati wa ku-employ watu tunaambiwa twende Kapsowar, ni mbali sana watoto kutoka hapa kufika Kapsowar wakati wanataka kuchukuliwa na serikali wanakua na njia kwa sababu wako mbali sana. Ningeomba station ya kuanjiri watu iwe pale na ni central. Kulikuwako wakati mwingine ambaye tulisaidiwa na serikali wakawaanjiri watu wa hapa Tot, na tuliona watoto wetu kweli waliaandikwa kazi wengi. Sasa hiyo shinda ndio tunaomba ile itasaidia sisi watoto yetu tuwe sawa na wengine, kwa sababu tunaona kama tumegawanywa mara mbili. Sasa ndio mimi naomba hiyo kabisa Serikali watusaidie sisi.

Ya pili, ningeomba Serikali kwa sababu hapa area, ni insecurity area, tungeomba serikali wasaidie wawape ma-chiefs (inaudible) ili shinda yeyote ikitokea, tunapeana mawasiriano haraka sana kwa Serikali, naona hiyo serikali wakitusaidia hii maneno ya security itakuwa rahisi, kuwezesha serikali kupeana report haraka sana, ili askari wakimbie haraka sana. Pia upande wa ma-chiefs, kwa sababu ni kazi ngumu, tungeomba serikali hata waombe ma-chiefs pikipiki, motor cycle ya kusaidia, wakiona shinda mahali iko, basi haraka sana wanakimbia hiyo maneno. Nafikiri yangu nitatoshea hapa nasema asanti kwa serikali.

Com.Lethome: Bwana Chief swali moja tu. Kuna watu wanasema ma-chiefs wawe badala kuwa wanateuliwa, wachaguliwe na watu, watu wanafanya mlolongo na kuchagua ma-chiefs.

Lawrence: Asanti sana, mimi ni mmoja ambaye nilifuatwa nyuma.

Com. Lethome: Sasa ungependa nini?

Lawrence: Ningependa, Serikali wapeane report ma-chiefs wafuatwe nyuma, kwa sababu, kumbe kuandika chief hata unaweza kuandika mtu ambaye hajui kuongoza watu kwa njia nzuri. Mlolongo ni mzuri kutoka kwa wananchi.

Com. Lethome: Asanti bwana chief.

Lawrence: Mimi ni mmoja ambaye nilifuatwa nyuma.

Com. Lethome: Caleb Fredrick, Caleb nawakumbusha watu ukija hiki kitu kinataka kunyongwa hapa kwenye shingo, ukishika kwa mkia kinafanya fujo, shika hapa kwenye shingo yake.

Caleb Fredrick: Kwa jina ni Caleb Fredrick ningetaka kugusia kuhusu marginalization ya huku kwetu. Mimi naona hapa Marakwet, naona wakati wa tuseme wafanyi kazi wa Serikali wakifanya huku, wakikuja huku tunaona wanafanya kazi na hardship sana. Na huku ukiona mtu mwenye anafanya huko Baringo ama penye tuko border nayo, wao wanapewa sana marupuru, kwa sababu ya kusema ni hardship, na huku tena ni hardship. Sasa tumeona kama sisi wamarakwet hatuko kwa Katiba ya Kenya kabisa. Sasa ndio ningeomba Serikali, wa treat hapa Marakwet kama nchi nyingine kama huko Baringo.

Na ya pili ningependelea kuhusu Judiciary Katiba ifafanue kabisa juu ya local courts, hii ya kinyumbani. Kwa maana tungeona mtu akifanya makosa hapa, hapa iko kitu nimeona kama ni jungle law, whereby offended on the other side anashikwa lakini tuseme wakija wakiua sisi, wakishikwa huku, wanapelekwa halafu ukifika huko kortini wanasema ah, hajaonekana akiwa he has not yet been gotten with any mistake, sasa anaenda scot-free. Lakini huku kwetu sasa mtu akipata wakiwa na criminal halafu tunashikwa inapita huku, mtu anaenda mpaka ananyongwa, sasa inamaanisha there is got two trials which of course is operating. Sasa tulikuwa tunataka kama tukiona kama ni Katiba, iwe Katiba ya Kenya mzima sio ati kusema huku Marakwet, huko huko, sasa ningependelea hii local courts hii ya wazee itambuliwe sana na sheria. Na pia huku kwetu kama zile services ya Judiciary iwe na mobile court. Resident Magistrate awe anatembea, ndio nayo iwe inapunguzia sisi kwa njia ya transport, kwa maana mpaka hapa Eldoret ni kali. Sasa mimi naona kama hiyo nimemaliza kwa upande wangu asante.

Com Lethome: Charles Kisigot, mwalimu.

Charles Kisigot: Naitwa Charles Kisigot, nitaongea kuhusu wasio bahatika katika jamii. Moja ni kina mama, walemavu,

watoto, waliozeeka sana, wagonjwa, wasiokuwa na mashamba, waliofiwa sana, sana, kwa ugonjwa wa ukimwi, wenda wazimu na walio maskini. Nataka katika Katiba ya nchi hii, iwe inawapa mamlaka wapewe nyumba bila malipo, ama wajengewe kama hawana. Vyakula vya kutosha, elimu, na afya wapatiwe uwanja na vifaa vya michezo ili nao washiriki katika michezo kikamilifu.

Katika kazi, job opportunities, wawe pia wanakuwa considered. Jambo lingine wawe wakisikizwa sasa kama siku ya leo walemavu hawako na sisi, kwa sababu wako milimani juu, hakuna Serikali ama Katiba haijapatia nafasi hata ile helicopter ingekuwa hapa ingetua pale juu, walemavu wote wafikiwe na watoe maoni kuhusu Katiba ya nchi hii. Jambo lingine, wapatiwe usalama, security, nao pia hawaoni hawawezi kutembea na wenzetu wakitupiga huwa wao wanaangamia sana, wengi wameuawa hapa. Hata tuna shule ya walamevu hapa Chesongoch mpaka sasa imefungwa, watoto wa shule hiyo hawako, kwa sababu hakuna usalama. Hiyo tunaona kama yule mwenzangu alinitangulia aliongea ninaona kama nimeshikwa na hasira sana, sababu tuna serikali mbili hapa, mashule upande vile, mashule upande huu lakini mashule upande huu inafungwa na ya upande ule in-operatate, hiyo ni mbaya sana.

Interjection Com. Lethome: Kwa upande ile ni gani?

Charles: Upande wa majirani zetu kama Keiyo, Pokot Magharibi, Baringo, Trans Nzoia mashule yao inaendelea, lakini hapa pengine juzi, juzi tu, ndio tukaja hapa haijapita hata miezi miwili. Sasa tunaona kama hata askari wakiletwa mtu alisema police waongezwe hapa, lakini haisaidii chochote maana hata mimi nimewahi kushiriki katika kufuata wale wauaji, ama wahamizi kufika mwisho wa wale wanatoka eneo hili, huwa askari wanasema oh, hiyo ni wilaya nyingine hatutavuka mpaka. Lakini hapa, sisi vijana tukiiba ng'ombe wawili hapa tulete upande hii, ma-helicopter, DC, PC, nani amekanyanga hapa na hata ma-chief wanashikwa, ma-councilor ndani wanawekwa ndani ya nini?

Interjection. Com. Lethome: Sasa mwalimu unapendekeza nini?

Charles: Napendekeza usalama tupewe, na Raisi ambaye aliye mamlaka katika wakati ule, awe akiwajibika sio kisiasa tu, bali kwa raia wote. Na Rais awe anashtakiwa na Serikali yake, kwa kutolinda mtu na mali yake, na pia mbali na kushatakiwa awajibike kulipa ile jamaa imefiwa, compensation in other words.

Jambo lingine ni kuhusu usalama, usalama wa kazi na usalama wa mwili. Hapa wanasiasa wanasema, chief umekuwa na mkutano, hujakataza wapinzani wake, wapinzani wa mjumbe yule, Chief usalama katika kazi yake uko mbaya, kama ma-chief wa hapa na ma-chief wengi, wamesimamishwa kwa sababu hawajafuata vile mwana siasa anataka. Nataka kuanzia mjumbe, diwani, Rais wa nchi awe kama amechaguliwa, awe Raisi siyo ya siasa but wa serikali ya watu, ili mtu ambaye amejiriwa civil servant yeyote, ma-chief hapa wawe na usalama katika kazi.

Kuhusu uchaguzi nataka katika Katiba ya nchi ya Kenya tuwe na uchaguzi mara mbili kwa mfano nchi jirani ya Uganda hutekeleza uchaguzi wao mara mbili. Kuna uchaguzi wa Rais, wajumbe wawe ndani na mawaziri wawe wakiwarisha Serikali wakati uchaguzi wa kiraisi unaendelea. Baada ya kumaliza pale tuje kwa ujumbe ili tusiwe na wasiwasi kwamba ooh, sasa wakati wa uchaguzi kila kitu kiko paralised, ma-ofisi imefungwa, DC hayuko ameambiwa aende asimamie uchaguzi sehemu zingine kama Kajiado ama kama Lamu, na huko ofisi yake imekaa mbila mtu kuwakilisha.

Jambo lingine ni kuhusu wafanyi kazi wa Serikali, nataka Katiba ya Kenya ibadirishe ile sheria ya kwamba mtu anapaswa ku-retire ama kupumzika baada ya kufanyia serikali kwa miaka akitimisha umri wa 55 uongezwe, maana ukiangalia hapa ma-chief wale bado unaona ni vijana, vijana na wamefikisha umri wa 55 na bado wana nguvu ya kufanya kazi, miaka ama umri usongeshwe kutoka 55 hadi 60.

Jambo lingine, ni kuhusu utawala wa mkoa, Provincial Administration upande wangu natoa maoni yangu kwamba hii itolewe, na katika sehemu fulani, fulani kama Location tusiwe na chief, sub-chief awe. DC na DO watolewe, mfano tukiwa katika Wilaya ya Marakwet tuna DC ambaye ni mwenyekiti wa Wilaya wa usalama, maendeleo katika DDC, yeye anakua mwenyekiti na tuna mwenyekiti wa county council, local authority sasa hawa watu wote wana mamlaka sawa kila mtu ana Land Rover yake kama 110 ama 109 na kila mtu ana ofisi. Hawa watu tunaona kama kuna duplication of responsibilities Hii, ingefaa tuwe na moja, awe akiwajibika. Sasa mara wanasema watu wengine councilor ame-insight watu, ananaswa upande ule anakuwa upande huo. Na pengine huyu DC, ambaye si mwenyenji wa pale is a foreigner, anakuwa entrusted na mali ya ile Wilaya muhimu sana, kama misitu. Napendekeza diwani mwenyekiti wa county council awe mwenyekiti wa Wilaya na nafasi ya DC iondolewe haitufai kabisa kwa maoni yangu. Asanti sana hayo yote ni maoni yangu nashukuru.

Com.Lethome: Asanti kwa maoni yako mazuri, bwana chief kuna swali, Commissioner ana swali anataka kukuliza.

Com. Bernard Njoroge: Umesema kwamba kwa ajili ya wale waliouawa na mali iliyochukuliwa, ungetaka serikali ipeane compensation. Hivi ni kusema kwamba Serikali itapeana compensation kwa ajili ndio imetuma hawa watu, au kwa ajili imekataa kuwapatia security, au kwa ajili inaungana na wengine kuwatatiza nyinyi kama kabila ya Marakwet?

Charles: Asanti sana bwana Commissioner, nataka niseme sababu yangu haswa ya kusema wale watu, wamefiwa ama wale mali yao zimebolwa wawe compensated wakati ule. Kama mwaka huu tutakuwa na uchaguzi, Raisi na wajumbe watachaguliwa na yule atakayeshinda, ataibeba bibilia ama kitabu kitakatifu cha korani juu kuapa kwamba atalinda mtu na mali yake. Sasa hii Serikali itakayoshindwa kulinda mtu na mali yake ihesabiwe na ilipe kama kortini. Sasa, kama vile tunashtaki hata waalimu wakiiba mitihani ama wakikosa kufanyia kazi shule, si wanashitakiwa na kuwa wanapatiwa fine? Basi yule anayeongoza awe anashitakiwa na alipe wale jamaa wamepoteza mali, kwa sababu alichaguliwa na akaapa kwamba atatekeleza wajibu wake wa kulida, hiyo ndio sababu yangu. Asante.

Com. Lethome: Asante mwalimu, Francis Kipken, halafu Benjamin Suter akae tayari.

Francis Kipken: Kwa maoni yangu, kwa majina ni Francis Kipken. Ningependa kutoa maoni kuhusu powers of the President. Ningeonelea zile powers huyu President amepatiwa ziwe reduced: Kw mfano, yeye inasemekana ni Chancellor of public Universities, ingekuwa afadhali kama mtu mwingine angechaguliwa kuwa Chancellor of our public Universitie. Ndio sasa huyu mtu apate kazi yake afanye kazi nyingine ya kulinda waKenya na mali zao yeye tena asiruhusiwe ku-appoint hawa senior Government officers kwa sababu aki-appoint, wale watu watakuwa wa-sing ile tune ya, President hatakuwa akifanya kazi yake kama anavyo takiwa.

Ya tatu, asiachiwe ile power ya ku-control Parliament, ama Judiciary ndio wale watu wafanye kazi yao vile inavyotakikana. Na tena asiruhusiwe ku-appoint watu kama Ministers, na Attorney General, tunajua huyu Attorney General ako na powers, nyingi sana ako na mamlaka kubwa sana na anaweza tu kufanya kitu kulingana na vile anaonelea Raisi angependa. Tena ningeonelea hii minimum qualification age ya President, iwe 40 na maximum iwe 60. Kuelekea 70 years and above, inaonekana kweli hawa watu hawafanyi kazi, wako ile tunaita after noon life, wangeenda nyumbani wapumzike pole, pole.

Kwa hivyo naonelea iwe 60 na ningependa tena niseme huyu mtu asiwe mbunge. Hapa Kenya yetu leo,ile mali yote ya serikali inapelekwa wapi? Mahali huyu President anatoka, kwa sababu yeye ndiye President mtu mkubwa sana. Sasa ukienda saa hii huko Baringo Central, kila mahali ni lami, kutoka Marakwet from the North to the South hakuna hata lami ndogo imefika hapa. Kwa hivyo hata ukienda mahali unproductive area wameweka rami, sijui ni ya nini na ni pesa ya WanaKenya wale ambao wanalipa taxes. Na yule President awe a University graduate with a degree in Political sciences. Na ningeonelea tena baadhi ya siasa yule mtu anakuwa President ana allow hii coalition Government, ndio tusiende kusema wale watu wengine ni watu wa upinzani, wale wengine ni wa Kanu, mpaka sasa tukawa na ile chuki kati yetu kama waKenya. Ni hayo tu asante.

Com. Lethome: Benjamin Suter.

Benjamin Suter: Mimi naongea kwa mamlaka ya county council chairman, ama chairman to the council. Nikiongea maoni yangu ni kwamba, apewe mamlaka kusimamia District na raslimali zote za District, kwa sababu gani? Kwa sababu tukiangalia maduka along the Valley, kutokea Arol mpaka Tot utakuta maduka zaidi ya mia nne imefungwa, na county council chairman, ana collect the tax katika haya maduka. Na haya maduka yamefungwa kwa sababu ya insecurity. Na kwa sababu wanataka kupewa mamlaka ya kusimamia mali, yeye angewahi kufanya hesabu angekaa chini na kufanya hesabu na kujiuliza ni kwa nini yeye hakatwi tax kwa nini haya maduka yamefungwa na yeye mwenyewe anafuata watu(inaudible) kwa nini amepata hasara? Mimi napendekeza apewe mamlaka ya kusimamia hayo kwa District, county council chairman.

Ya pili, ni mambo ya food and security: hapa Kerio Valley nimeonelea watu wote walishwe wapewe chakula na Serikali. Sababu gani? Kwa sababu sio ati tumekosa mvua ama nini kwa sababu walikuwa waki-sterve hawakulima? Hali ya

Gabriel: *Ko kisome cho serkali amun ele koroni ni motinye chi mali, ne motinye chi mbar nyo bole, ko momi ole teptoi ko kazi bure mbo lagoi choto*

Translator: Tunaomba Serikali iturejeshee usalama ili tufanye kazi halafu mambo yote ya famili kusomesha watoto, kulisha familia iendelee vizuri.

Gabriel: *Ko momi nye tomwoei ane, moche kepa ak ketibi nya karam ko momi che kosumbuonon mukatenyun, sotou kasit nyun amun bichon markweta, kichome kiipchigee kesomesanen lagochok, ak kebal mbaret chok, mukimure ng' olion age tugul. Momure buchongo chii kasit nyo nyonet.*

Translator: Kwa maoni yangu ya mwisho ningesema mimi kama Marakwet napenda kusomesha watoto kufanya vitu vyangu ya mkono. Ningependa hasa nikae kwa usalama, nisisumbuliwe tena, hiyo iwe ni wajibu wa Serikali nikae kwa usalama nifanye kazi yangu. Asante.

Com. Githu Muigai: Hili swala la usalama, wewe ukiulizwa kama mzee ni kitu gani Serikali inaweza kufanya kama wiki ijayo

ndio usalama urudi hapa kwenu?

Gabriel: *Komurenjon chon serkali, koswa kile nee ne kasumbwanech. Kowirta tugucheb tinye pokot ketebi eny karam.*

Translator: Tunataka Serikali ione ya kwamba ni nini inawafanya hawa Wapokot kuja huku wachukuwe silaha zote ambazo ziko huko halafu tukae kwa usalama.

Com.Githu Muigai: Na silaha ya Wamarakwet sasa tufanye nini?

Gabriel: *mokitinye cha tugul kii*

Translator: Sisi pande hizi hatuna.

Com.Lethome: Yule mama, can we have a lady? Ulikuwa umejiandikisha, tunaruka kwa kina mama kwa sababu tunajua mmechelewa kwa sababu na mnaenda nyumbani mapema kwa sababu ya kazi. Peana jina lako mama.

Josephine Kipkeo: *Ng'ala motinye che chang, olen kongoi en serkaline koip katiba konyo olibo legem.*

Translator: Sina kitu cha kusema, sikuwa natarajia hata serikali itakuja mpaka upande huu ni vizuri mmekuja saa hii mmeanzia sehemu za chini ili muanze kazi kama Serikali

Josephine: *Achek biich ab markweta kekere serkali ko kokosop kemoche siko toretet biich chebo markweta*

Translator: Kama Serikali ilikuwa ile tumeona sasa, sisi kama Wamarakwet tunaona hii nchi yetu imeanza kupona.

Josephine: *Koroni komo koret, kisome serkali kowek kaliet kile zamani*

Translator: Hii nchi sisi hatuoni kama ni nchi pa kukalika, kama Serikali bado mko mturudishie hali ya hapo awali

Interjection Com. Lethome: Kwa nini haikaliki?

Josephine: *Momi kii ne kiwech koroni kou kimukon*

Translator: Hakuna kitu kimeharibu nchi hii kabisa kuliko Mpokot.

Com. Lethome: Sasa unataka Mpokot afanyiwe nini? Serikali ifanye nini kwa huyu Mpokot?

Josephine: Kama Mpokot kama nyinyi nataka kuona mtu yule baya ama kama mtoto wangu yule mimi nazaliwa kama naona, ni mbaya kukanyaga hata kama mimi halafu nakaa nje, nje, kukanyanga kama mtoto ni mbaya ama ni yangu chapa kabisa.

Com.Lethome: Sasa tunasikia Wapokot wako na silaha, sasa unapendekeza nini kusiwe silaha kwa Wapokot na ile ya Wamarakwet?

Josephine: (inaudible)

Com. Lethome: Na wanatoa wapi hiyo silaha wako nayo?

Josephine: Sijui nani atajua hiyo?

Com.Lethome: Sasa si kuna police hapa? Sasa wakati Wapokot wanakuja kuvamia, police wanafanya nini?

Josephine: Sijui police wanakuja tu pole, pole, sasa kufika hapo (inaudible)

Com.Lethome: Sasa unataka tufanye nini sasa, kwa sababu Serikali imekwambia sema tutakusaidia vipi? Sasa tunataka useme unataka nini sasa?

Josephine: nyinyi mtaweza kuona kama mimi nakuja leo, nakuja kesho, nyinyi mtachunguza. Mjue mtafanya nini.

Com.Lethome: wewe unataka tufanye nini?

Josephine: Mimi nataka (inaudible)

Com.Lethome: nyingine.

Josephine: (inaudible) habari ya fees, Serikali waangalie watoto, halafu watoto hapana lala, tupate tu kidogo kidogo (audible)

Kimoche President ne toreti biich

Translator: Yule President ambaye mnataka kumchagua kama waKenya, tunachagua yule ambaye anaona kila mtu atendewe mema.

Josephine: bado hiyo tumelia zaidi kwa (inaudible) lakini kama hii ni (inaudible) sijui tutafanyia nini watu kama imekuwa mbaya watu wote. Sasa (inaudible)

Com.Lethome: Sasa President ni MP ya sehemu fulani kwa mfano President yeye ni MP wa hapa Baringo Central, sasa ungetaka katika hii sheria mpya President awe pia ni sehemu moja ama namna gani?

Josephine: President ile original, ile iko national hapana ya pande hii, ile ya national itakuwa ni ile imengalia kabisa. Halafu nafanya kitu, kama mimi nafanya kitu yangu hapana nyanganywa kwa ndani ya nyumba, kama mimi niko na kiosk yangu kidogo hivi hapana mtu kuja kunyanganya mimi, angalia hivyo hivyo, kama baba yangu ako na mbuzi mbili, jabazi asiye akaninyanganya, hiyo ni mbaya kabisa, angalia hiyo, hiyo kabisa, kwa nchi yetu. Kama hii nchi ni yetu, tuangalie nchi yetu kama yetu. sivyo ni hiyo wananchi mimi nawambia. Angalia kama mtu ako na mbuzi mbili, wacha achunge halafu itakuwa ya watoto wake. Kama ni moja iwe ya watoto wake. Wacha kuchuka kama napata ile mtoto wake mdogo, mwingine nakuja chukua mimi nalia tu hapo. Hiyo ni mbaya ndugu kabisa, hiyo ni mbaya sana.

Com.Lethome: Tupatie majina sister.

Sister Francisca Khaesa: Kwa majina ni sister Francisca Khaesa hiyo ni majina yangu. Niko na mambo machache natoa maoni yangu kibinafsi, na ni yale yamesemwa sio maoni mapya. Kwanza naanza kuongea kwanzia na Bunge. Mimi ningependekeza, mbunge yule tumemchagua awe na boma yake katikati ya watu. (inaudible) ikiwa una sherehe fulani, ana andamana na mama wa kwakwe kwa sababu uongozi una anza kwa mboma. Tunajua kuwa Mbungeni siku za mbunge ni tatu, kule mbungeni siku ni tatu jumanne, jumatano, na arahamisi. Tungependa mbunge siku ya ijumaa, jumamosi, jumapili tujue mahali ako, akuje ofisi mahali pale, pale tulimchagua. Twende pale badala ya sisi kuchanga pesa kuhusu kuuza mbuzi sisi twende huko ofisi, ya Mombasa, Nairobi kwenda kumtafuta halafu kwenda kupitia kwa secretary wake ni ngumu, kupitia kwa rafiki yake kumpata ni ngumu.

Tunataka yule mbunge tunajua wiki hii, ako Location gani hapo ndio atakuwa na ofisi yake akiona watu na yale maoni tunampatia anapeleka Mbungeni jumanne, tunasikia kwa mukhustari wa Mbunge jioni, tunasikia Mbunge wa Marakwet alikuwa akipeana maoni kuhusu watu wake aliyopata huko nyumbani weekend, hiyo ndiyo tunataka. Na hivyo hivyo councilor awe hivyo, hivyo ama diwani tunamchagua tu tunamona pale, pale kama ofisi inaanza saa mbili mpaka saa kumi na moja, tunamuona kwa ofisi kwa sababu ile pesa wanalipwa ni pesa yetu, sisi tunalipa tax tunatoa kodi na hiyo ni mshahara yao ingawa wanajiongezea bila kutuuliza, sisi tumewadika kazi wakifika kule wanakua juu yetu, tunataka tumewachagua wakuje pale wafanye kazi.

Com. Githu Muigai: Sister kabla hujatoka hapo kwa mshahara, in future ungependa tufanye nini na mishahara ya watu wa

bunge?

Sister Francisca: Mimi ningependekeza kuwe na committee ama commission ya kuangalia mishahara ya hao watu, na hao watu wa kuangalia mishahara wachaguliwe na watu na waende wazungumziwe bungeni, na yule President afanye endorsement sio wao kwenda kujiongeza wenyewe. Labda waongee wazungumzane ni huyu, ni huyu, na wanalie file yake vizuri halafu, President aseme watu wamesema ni huyu, na huyu amue mishahara ya hawa watu sio wabunge na wale wengine. Halafu tikishaingia mbunge, diwani hata chief, chief akae na watu saa ingine kama unasikia kuna mgologolo mara ingine maneno inatokea tunaambiwa tukimbie kwa chief, chief ameenda safari ameenda mishahara wiki mbili, hapatikani halafu watu wanahangaika wana kaa kama kondoo bila mchunganji, sasa tungependa kama hayuko ofisi tujue nani yuko ofisi kwa sababu hata ile pesa wnaapata mishahara yao ni pesa yetu tunawalipa na kama hatuwalipi wakatae kazi. Ningependa kwanza mbunge tunaye chagua

Interjection Com Lethome: Sister wacha ni ku-interrupt. Habari ya chief umesema analipwa mishahara na wananchi lakini sio wananchi waliomchagua, ungependekeza nini katika Katiba mpya, chief hamkumchaguwa, hakuchaguliwa ma chief wanachaguliwa kutoka katika office of the President ungetaka tuendelee hivo ama vipi?
ungependekeza nini ungetaka tuendelee hivyo ama nini?

Sister Francisah: Mimi ningependekeza wale wanaenda kufanya interviews hiyo majina irudishwe kwa wananchi, iangaliliwe kwa wananchi. Kuna wazee wanajua hawa watu, washirikiane na watu wa special branch wazungumze na wanalie ma file ya hawa watu walisoma wapi, walikuwa wakifanya nini wakati huo wote, na wachunguzwe vilivyo, kwa sababu watakuwa wakiangalia maisha ya watu. Mtu aliyekosana na bibi yake anakimbia kwa chief, mtu aliyekatiwa shamba yake, mtu aliyeimbiwa anaenda kwa chief. Chief anaaminika, ni Mungu wa kijiji, kwa hivyo kama sio mwaaminifu shida iko Kwa hivyo ndio nasema hawa chiefs wawe ni watu, watu wanaishi na watu na tunawaamini.

Ningependa elimu ya mbunge, ya diwani, na ma chiefs also iangaliliwe. Pale mbunge awe ni mtu alisoma, kama amesomea mambo ya Agriculture, pale kwake ionekane ni mtu ako na degree ya ukulima, kama ni mtu aliyesomea mambo ya Engineer kwake ionekane kuna barabara, kwa sababu akienda kule anajua kutetea. Kama ni mtu aliyesomea mambo ya mifugo ama ni mambo a kibiashara pale kwake Constituency yake biashara ivume, ieleweke, kama ni hivyo, awe amesomea na ako na cheti cha pekee. Mambo ya diwani machiefs wawe angalao wameanzia kidato cha nne na kwenda juu na kosi ya kipekee, ndio wakienda kule kama kwa council, tunasikia kuna finance, kuna nini, mtu anajua mambo ya account, pesa ikiingia ile imegawa na Serikali ikiingia pale accounts zinatoka zikiwa sawasawa. Hiyo ndiyo maoni yangu kuhusu mbunge, diwani na chief.

Ile nyingine kuna hii distribution of resources. Unaweza kusikia ama tunasema kuna shida tupewe mahali tuende tukae, kama kuna shamba imetolewa mahali ya wasiyo na shamba. Ningependekeza hiyo shamba viongozi wasipate igawiwe wale wasio na shamba, lakini sio kiongozi kwanza kwenda kama ni wananchi wanakatiwa acre 5, yeye anajikatia 50. Kiongozi asipatikane na

kipande cha hiyo shamba na hasa kuhusu pesa tunasikia kuna pesa zinaletwa za kuhusu mradi huu, na huu, na huu, hatujui kiasi yake nani alipewa na ni za wananchi, kuwe na committee kwa kila District ama kwa kila location kama kuna pesa zimetoka kule sijulikane zimekuja distribution imefanywa namna hii, watakao shughulikia hizo pesa ni hawa na hawa na watote wakati fulani wakuje wambie wananchi pesa imekuja namna hii, tulitumia namna hii, halafu kuwe na accountability na watu waelewe. Kwa sababu hata kama wanatumia vizuri, watu wasipojua watasema wewe ni mwizi ndio kuwe na uaminiani.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya afya, tuangalie kwa District yetu, District zingine zina mahospitali kubwa, kubwa. Angalao Serikali iangalie kwa kila District kuwe na District hospital ile watu wote wanaenda pale, kuna madaktari pale. Hata tunaomba madaktari watembe kule vijijini waone watu. Na kuhusu mambo ya afya hapa kwetu tuna wataalamu kabisa, wanaweza kukupasua kichwa, kwa nusu saa na kukuunganisha na baada ya siku mbili unaweza kutembea. Mimi ningeomba hawa watu wapewe nafasi ya peke waende waangaliliwe wasaidiwe mambo madogo madogo ya usafi kuangalia mambo ya wakipasuwa mtu awe waungane watu wa wale madawa halafu walipwe na serikali.

Interjection Com. Lethome: Wataalamu wa kienyeji? Wanawesa kukupasua kichwa?

Sis. Fransisca: wa kienyenji, wanapasuwa kichwa na kukuunganisha na unatembea. Kama wako waangaliliwe mambo yao (inaudible) wanafanyia kule chini ya mti na mambo yao, wagawiwe mbuzi mbili na mtu amepona na huyu angepelekwa Kenyatta, ungesikia harambee ifanywe, si ndivyo? Harambee ifanywe tuchange, nyinyi donors waitwe, na kule unaeda unawekwa mlolongo unambiwa utapasuliwa baada ya miezi mitano kwa sababu watu ni wengi. Kwa hivyo hawa watu wako hapa tunaishi nao, ndio sisi hatuedi huko Kenyatta tunamalizia mambo yetu hapa. Hawa watu wasaidiwe na wawekwe mahali wanaweza kupatikana kwa urahisi, hilo ni pendekezo langu. Kwa sababu tunao watu hatuhitaji madaktari, tunawahitaji kwa ujuzi kidogo, labda ya kuponyesha kidonda tunawahitaji kwa hivyo tungeomba hawa watu wachunguzwe.

Ingingine ni maendeleo ya pombe, pombe kwetu imefanya maajabu. Pombe imefanya majaabu, tunalia Wapokot, Wapokot, lakini kuna Wapokot hapa kwetu inaitwa pombe ukweli au uongo?

Audience: Ukweli.

Sister Fransisca: Ndio hiyo pombe tuangalie nani anasimamia kijiji achunguze maneno ya pombe, hata kama kuna (inaudible) tumesema turuhusu pombe ya mtoto, ya kupatia mtoto jina, pombe ya harusi kidogo, kidogo, lakini hii ingine nikitaka kwenda kuona chief, naenda na corporals naenda kidogo akunywe ndiyo tuelewane. Nikienda kwa councilor, councilor ninampeleka kado akunywe kidogo ndio asikilize, na pombe zingine ati nisomeshe mtoto ningeomba serikali itupatie nafasi ingine za kuweza kusomesha watoto, za kuweza kujinua kifedha lakini sio pombe, imagine mwalimu amepata mshahara yake anapitia kwangu, nampatia pombe anapatia mimi noti 1000 namwambia ni 100 kwa sababu haoini vizuri, watoto wake hawaoni kwake haoni, sukari nini halafu tunauana sisi wenyewe, hata afadhali, hizo pombe zipigwe marufuku, kama iko pombe ieleweke kwa sababu

watu hatakosa kukunywa, ukweli ama uongo?

Audience: Ukweli

Sister Fransiscah: Watakunywa na wakunywe ile pombe medicated pombe zingine zinana. Tumepoteza watu kadhaa shauri ya pombe peke yake, kama ni pombe na mtu amekunywa pombe, nimesema kama mimi nimepika pombe mtu amekunja kunywa pombe yangu, na ameenda amekufa mimi nitwe niende niangalie hiyo maneno ni mimi nimetengeneza hiyo pombe. Kwa hiyo ningependa hiyo sehemu kwa sababu ma chief wako na sisi waangalie maneno ya pombe imeumiza watu wengi. Familia zingine zimevujika shauri ya pombe.

Ningesema ingine kuna hasa ile inaitwa legalized abortion, kuna abortion tunafanya hapa kwetu, kwa kitamaduni yetu tunasema mimba itolewe nini na nini, mtoto anakufa nini, na nini, mimi ningesema anayesaidia kufanya hiyo abortion ama utoaji wa mimba na mwenye kutoa mimba na wanao shiriki wote, wote wanaswe wawekwe ndani na wahukumwiwe kama wale wanaua watu, kwa sababu watu wamepoteza watoto wao kwa kujua ama kwa kutojua. Tunawajua watu tunaishi na wao na unaenda kwake unakuta aka (inaudible) Jumatatu nani anakuja, jumanne, mpaka jumamosi watu wako pale wanatoa mimba. Niko sawa, kwa hivyo ningependa hiyo maneno serikali itoe amri kuhusu hiyo maneno, kama hii maneno imetokea tutafanya nini.

Ingingependa mambo ya wa mama, kwa kweli ukiangalia hapa, utafikiria hii nchi ni ya wanaume tupu, lakini ukienda kule nyumbani wamama wako ama sivyo si wamama wako, lakini kukuja kwa mambo kama haya, wanaume wanajipeleka mbele, hata mtu hawezi kuambia bibi ya kwake au mke wa kwake tuandamane twende tupeane maoni yetu, na hiyo ndio inatuweka nyuma, hata ukija hapa labda unaogopa ukisema hii, na hii, ukifika kwako fimbo inaongea ama mateke inaongea, ulienda kusema nini? Hiyo ndio wamama saa ingine wanaogopa, labda wale wameongea pale ni wale wazee kabisa hakuna mahali unaweza peleka yeye. Lakini utakuta kwa mara nyingi, wa mama hawana uhuru utakuta kwa baraza wa mama wamekaa kado, halafu baada ya kumaliza utasikia mama moja asimame aongee kwa niamba ya wamama wote, mama moja tu kama ako na kitu ya kusema aongee asionge, hakuna maneno, hiyo ndiyo nimeona kwa zile baraza chache nimehudhuria.

Intejction Com Lethome: Sasa ungependekeza nini hiyo?

Sister Fransisca: Ningependekeza zamani hapa zamani wale walikuwa zamani, baraza ya chief hata kama uko na mtoto mgonjwa ulikuwa ukipeana report, nitapereka mtoto hospitali, na nikitoka huko nitakuja kuhudhulia baraza. Ilikuwa kuhudhulia baraza ya chief ni kitu kubwa na sijui imekuaje, unakuta chief ako na baraza yake, watu wanafanya mambo yao, watu wanafanyia tinga huko wanachanga mahindi hawahudhulii, na unakuta chief ako na mambo ya kueleza watu pale mafunzo ya wananchi pale watu hawahudhulii. Nafikiria pale wamama wangukuja na waongee kwa baraza ndio mambo yao isikike pale.

(noise from the background)

Sasa ile ningesema yangu ingesaidia, tuangalie elimu ya wasichana. Elimu ya wasichana labda ndio itaweza kusaidia. Utakuta wasichana, mvulana kwa nyumba hata kama msichana amepita zaidi utasikia angojee kijana apelekwe shule, halafu mwaka ufuatao kama pesa itapatikana atapelekwa shule, halafu hiyo itakatisha moyo. Ama utakuta msichana amepelekwa ile shule ya karibu na kijana amepelekwa shule nzuri, na hata shida nyingine kwa District yetu hatuna shule ya wasichana, hiyo ndio ningomba Serikali iangalie, wakati wa kugawa hizi hii keki ya nchi yetu tugawiwe keki ya elimu ya wasichana, shule. Ili wasichana unaweza kutuma pale na wakitoka pale tunatagemea viongozi wa kesho unajua ukielimisha mama mmoja umeelimisha jumuiya yote. Ukielimisha mwanamme, umeelimisha mtu mmoja, hivyo ndio ukweli wa mambo. Kwa sababu mama asipo ng'arang'ara, hata mzee hatang'arang'ara, mama aking'arang'a boma yote inang'ang'ara, kwa kielimu hiyo ndio maoni yangu.

Ile ningependekeza nyingine kuhusu wasichana, tuko mara nyingine sehemu zingine kuna hii inaitwa kutahiri wasichana. Mimi ningependekeza hiyo wale wangependa, miaka isongeshwe mpaka kumi na nane, anayetaka kuamua ajiamulie pale kwa sababu kwa kimila yetu mtu akienda hii sherehe akitoka pale alikuwa aende kuolewa, ukweli au oungo? Si ndio anaenda kuandaliwa kwa mambo ya kwenda kuchunga boma yake, lakini unapereka mtoto wa miaka tano anaenda kuchunga boma ya nani? Ama anaenda anandaliwa kwenda kuolewa na nani? Sasa hiyo ningomba hiyo tuchunge, mtu awe na miaka ya kutoshea ana amua anaelewa mambo yote. Kwanini anaenda na madhara yake na uzuri wake aelewe, ndio akiamua mwenyewe baadaye hasemi mimi si kupenda nililazimishwa baadaye hakuna kusema ningejua, hiyo ndiyo ningesema mtu akifika miaka 18 awe ameelewa.

Kingine ningependa kusema wale wanaochagua kwa kura ya siri, unachagua kura ya siri saa zingine hatuelewi mtu. Kama tumechagua mbunge au councilor na ameenda pale, mwaka mmoja huko na miezi kumi na mbili, kama kwa huyo mda mwaka wa kwanza, kama hatujaona kitu, kama tuseme wakati alikuwa akiomba kura yake, alikuwa akisema mkinichagua nitawawekea maji kwa nyumba nitaweka barabara kwa kila mlango ya mtu, nitawaletea stima hata jikoni, sasa hivyo vitu vyote baada ya mwaka mmoja kama hatuoni hata moja, forum iitwe, ile forum alikuwa akiombea kura ikutane tena iamue hayo maneno. Tunaweza kuchagua mwingine kwa sababu ni sisi tume mwandika kazi, na hivyo, hivyo iwe diwani, ndio tukitoa wa kwanza wa pili akiingia ajue tuko serious ndio afanye kazi. Na tunatakiwa tuwe na evidence sio kumtoa kwa sababu sio wa boma yetu, ama kama tuseme hata kama ni mbaya ni yeye tu wacha akure, kwa sababu tunaumia. Ile shilling ishirini tunakula kwa kuombewa kura, shilingi ishirini na kuweka kidole tunasema tukae bila barabara, bila hospitali, bila masomo, tupigwe na pokot sasa hatuwezi kulalamika kwa sababu ni sisi tulichagua, sivyo tunalea kiongozi mbaya lakini sisi tulichagua, kumbe tuko na uwezo wa kumtoa tukitaka, lakini kama tulikula, kula tunasema pesa yake labda itaniroga nini nini, hakuna hiyo ni pesa yetu. Nafikiri kwa hayo machache ni hayo, naakika kama kuna swali yeyote, niulizwe.

Com. Githu Muigai: Thank you very good presentation, Micheal Kiptoo uko kuja, afuatwe na Wilfred Kipkeu, Wilfred Micheal uko wapi?

Micheal Kiptoo: *kii ne omoche amwa ko okobo koret. Kisumbuanech kisumbuanech mukonindoni ago kikimii tugul*

ng'ung'u nyande ago ye nyo kiro kele kole kokipoi kiburion ko ta ko baratech ago mo kikere ng'olion ne kikitou en ng'ung'unyandet. Kochochi ng'alek cho kitou ago bicho ko waskini mu koroni kobo

Translator: Sina kitu cha kusema ila tu nimeomba usalama huyu Mpokot tulikuwa na yeye nilimlisha, na anazidi kutuumiza sana tunaumia sana kama Wamarakwet na umaskini umezidi sana.

Micheal Kiptoo: *ko ngo utat ng'o chichon len kere ko mo marikta yun keteben karam si ketupchi yu koronyon karam ak iomisye kiliyukinye ak momete che nyalul kole nomu chi chok kerire chi nyolel ne. Kelech jehova kongoi to ko chi tugul ngwo nye karam.*

Translator: Sisi kama wamarakwet tuko tayari kuungana na yeye tufanye kazi kama hapo awali na tunasema serikali itusaidie kufanya hii kazi ili tuweze kuishi kwa usalama.

Micheal: *Ko kelech Jehove kongoi amu akwek chebo pokot ko mo serkali, kotoretan mungu amu korenyun ne kikekwai. Ko kelenji jehova kongoi ketebi en korik nyo karam ak ke tweekhine. Jehova kimii ak ke rotu ke kong, ak ke ng'olole ko ngony nye karam ak kerutoi gaa nye karam ak kerutoi kotugul nye karam.....(inaudible)*

Translator: Tutashukuru sana kukiwa na usalama, mtu atembe mahali popote aendapo, tuishi kwa pamoja kama hapo awali mtu aendele na mambo yake kama vile anataka. Sisi tuko tayari kuungana na huyu ndugu yetu tufanye mambo kama vile tulikuwa tunaishi hapo awali, nashukuru sana.

Micheal: *Ko kole kongoi keteben korin chok karam ago motei irute wivu, ngo kowendi bichuto ngo kotewendi iwe inye karam, okiomishe en korinyo karam akimuch imuny ko tienge inyende ngo borto ngung ko kongoi ngo cho tugul kele cho kongoi kabisa.*

Translator: Tunasema kuwa kusiwe na wivu kutoka kwa mtu fulani, kuwe marakwet au mpokot kama mtu ako na mali yake, awe nazo na iwe ni yake sio ati kuja kunyang'anyang'a twashukuru sana kukiwa na uvumilivu mtu awe na mali yake, kusiwe na mambo ya kuja kunyang'anyana mali.

Micheal: *Kelen kongoi neko keterchine en kori nyon karam ketorchine ago kebir kongoi ango sobondonyun kele kotestai sobon nyon nyo karam .*

Translator: Tukizidi kuana hakutakuwa na faida, kwa hivyo tungependa kuishi kwa usalama na tuweze kuendelea mbele kama watu wengine.

Micheal: *Ko kelechok kongoi amun akwek serkali.*

Translator: Nimeshukuru sana.

Wilfred Kipkeu: Yangu nikuanzia kwa maoni yangu ya President, Rais wa Kenya awe the term to be extended from let us say for example 7 years or 10 years. Why? Because since 1992 because of multi party the economy of Kenya has it has come down because the Government is using money for campaigning every 5 years, and you must accept that. That is the the point, so the President should according to me, awe tu akae miaka kumi, sio miaka mitano kila siku pesa pesa, mchango. Tena wakati huu President amesema atafanya mchango wa kupata pesa ya ku-campaign, you must know that. Maneno ya Wapokot na Wamarakwet ngonja niwaambie nyinyi ukweli. Kuna kimila ya Wapokot inaitwa sabana. Katika sabana unaambiwa kama umeua mtu wewe uko na cheyo kubwa katika hiyo sabana. Hiyo kimila ya pokot tena pokot wamesema sisi wamesema tutaedelea kuua turkana, kuua marakwet kama sisi bado tuna lipa dowry. Hata wale police officers wanaomba risasi wanakunja kuua watu hapa wanatafuta mali ya kulipa msichana. That is the problem because I have stayed with them and I know the culture in and out, so I am (inaudible)

Com.Githu Muigai: Ngonja kidogo nikuulize swali hapa. Tukitoa amri wasichana wapeanwe bure na wapokot unafikiri wataacha kusubuwa watu wengine?

Wilfred: Wataacha na kule Wapokot wamesema kama mtu ako na wanawake zaidi ya tatu wewe unaangaliwa kama mfalme, wewe ni mfalme wa nchi. Sasa mimi nataka ninapo maliza maneno ya hapa tuko Kerio Valley, nimeambiwa hata kule Nairobi nimewahi kutangazwa mara kadha, since 1963 hawajafanya land demarcation here from town here to their boundaries. The Commissioners, watu hapa wakishikwa hapa hawana title deed ya kortini, wanaenda kumia tu kwa ile inatwa equality of men, hakuna title deed. Kama juji juji wengine waliambiwa lipa 300,000 or give us a log book or you remain (inaudible) so nyinyi mpate title deeds. So you have to get title deed hata title deed unaweza kutumia kuomba loan halafu watu tajiri mnaenda kulipa school fees. Hata point for hii Female Genital Mutilation in Marakwet, wanapendelea sana wanaume waendelea na mila zao, because we are the jews in Kenya so we follow Jesus Christ was circumcised Women they are not supposed, that is their choice(laughter)

Rogo Rotich: Kwa majina naitwa Rogo Rotich ningependa nitoe maoni yangu kwa Kenya yetu kwa maneno mawili. Kwa upande wa election, wakati wa kuchagua watu, tunataka kama mwaka huu ni mwaka wa siasa halafu baada ya miaka tano tujue tarehe ya miaka tano baadaye ni lini, sio kitu tu President anajiwekea, inachuchunguza watu kichwa katika Kenya, watu wanasema tarehe itakuwa lini? Let us be specific (inaudible) so included in our review. Inginge ambayo tunataka kuchangia ni kuhusu siasa ya mashamb katika hapa kwetu bonde la Kerio, tuko na zaidi mizozo ya mashamba na tunataka wazee wawe the last solution, the final people to decide the (inaudible) sio kama wakati kama DO akikuja anasema, shamba ni ya huu na DO ni mtu wa kuhamishwa kupata transfer na sisi wa marakwet tunabaki. So ile suruhisho ya wazee tufuate kama hapo awali, na

maisha ikiendelea (inaudible) halafu hata hii maoni ya pokot isapishwe kama tukiwa na mashamba yetu (inaudible) na hakuna mali mtu sio kama hii huwezi . So this issue of title deed will be (inaudible) with this Kerio Valley people so that the lifes continue.....otherwise thank you for listening.

Com. Githu Muigai: Next ni Thomas Chemai, afuatwe na Wilson Kibor Njoroge, wapi bwana Njoroge, kuja karibia hapa mbele kiti ni yako endelea bwana Thomas.

Thomas Chelule: Jina langu naitwa Thomas Cherule. Mimi ningependa kutoa maoni yangu kuhusu mambo ya usalama. Sisi hapa mara kwa mara, tulionana na DC alikuwa hapa juzi ma DC wanataka tu kutoka Baringo, West Pokot na Marakwet na walisema ya kwamba, ng'ombe akiimbiwa moja hapa inaleta ng'ombe tano. Na mpaka dakika hii hizi ng'ombe hazijalipwa mpaka wa leo, na mtu akiuwa inalipwa ng'ombe 40. Juji tu wakati DC ma DC, waliodoka mtu mmoja akauawa na kuchukua ng'ombe yake, na hakuna kitu na hakuna hata yeyote mpaka saa hii ambaye amechukuliwa. Sasa tunataka Serikali wachukue watu wajue kwamba kama unataka kusaidia sisi, wasaidie sisi kwa njia mzuri.

Jambo la pili, ni kuhusu mambo ya maji ya Kerio, tunataka serikali wasimamishe maji ya Kerio ili wapatie sisi tutumie kwa mashamba yetu hapa chini. Hapa kwa sababu hiyo maja inaenda mpaka Labruto tena faida yeyote kwa sisi, na hiyo moja inatoka kwa msitu yetu hapa.

Intejction Com.Githu Muigai: Na hapa chini watakunywa nini?

Thomas: Watapata maji tu, maji yatafanya irrigation na maji itaenda hatukatalii hawo maji, tutapatia nafasi ya kupata maji.

Tatu ni kuhusu mambo wabunge, mbunge akiwa anaenda Parliament wakati huu na yeye hajafanya kazi, ile ambayo inapendeza sisi, baada ya miezi tatu hata mwaka mmoja, tunataka aondolewe aende ili mwingine aende ili atufanyie sisi kazi. Akitaka kusema tutatengeneza barabara, natengeneza mambo ya stima, au nini, na hicho kitu hakuna kumbe ni mdomo tu, na yule mwananchi wa kawaida bado anataabika na yeye anaitisha pesa tu anakula anakunja kunidanganya mimi na mambo ya barabara, sisi hapa tumesahauliwa kabisa, ingawa hata kama nyinyi rami mwaka uliopita, hii barabara hungepitia hata saa hii ingekuwa hii ni misitu tu basi sisi tunataka barabara iwekwe lami na Serikali kupitia hapa mpaka Turkana ili aende kuelekea huko Sudan. Hii ni barabara rahisi sana sio barabara ngumu. Hata juji ilifanywa tu kwa mda wa miezi sita hivi ikamalizika lakini kama ingewekwa lami, pengine matingatinga ishirini ingefanya kazi na ingemaliza kwa miezi miwili ama mitatu. Tena ni kuhusu mambo ya nyongeza ua mishahara ya waalimu. Waalimu wametaabika na wameomba pesa, na si waalimu peke yao ni watumishi wote wa Serikali. Kama mtu anapata tatu ama elfu nne, elfu nne siku hizi ni pesa gani katika Kenya hii ni Kenya ingine, hii hapana Kenya ile ya zamani si ninataka

Interjection Com. Githu: pendekeza mzee.

Thomas: sisi tunataka mishahara ya waalimu iongezwe kufikia 25,000 kila mwalimu, bora amehitimu course yake ya kutosha.

Com. Githu: hiyo tumeandika,

Thomas: Ingingine ni kuhusu mambo ya forest, sisi hapa tumefukuzwa fukuzwa na Wapokot tunafukuzwa na watu wa forest huko tukiwa na sehemu kidogo ya land kidogo huko wanasema tuko ndani ya forest, na hii forest ni yetu sisi hatutaki kuchafua forest tunataka tayari tukipatiwa kidogo hiyo kidogo, hiyo kidogo ndio iwe yetu, na sisi tukifanya polepoke bila kelele yeyote, hiyo ndio sisi tunataka.

Jambo lingine la mwisho ni mambo ya health, hapa imesahauliwa kabisa sisi watu wa hapa hatuna hospitali mzuri hakuna madaktari isipokuwa tuko na madaktari kidogo, kidogo hii ya badia pengine halafu na wengine ndogo, ndogo ambaye hawezi kusaidia chochote, kwa hivyo tunataka madaktari waletwe hapa kama chesongoch ama Tot health centre ili watumikie sisi kwa njia mzuri . Basi kuhusu madaktari ya nyumbani kama vile sister alikuwa anasema tuko na madaktari yetu ya nyumbani ambaye wanafanya mambo clinic ya mzuri, anasaidia watu kichwa wale wanaumia kichwa wameanguka pengine kwa miti sijui wamefanya nini, na tungetaka nyinyi serikali itoe usaidizi kwa hawo watu ili wafanye kazi vizuri na sisi. Kwa hivyo asanti.

Com. Lethome. Asanti sana mzee, ebu tupatie kina mama sasa, Njoroge ulikuwa umeitwa Kibor? Wilson Kibor Njoroge, tumpate Mrs. Albina Chemtoo.

Albina Chemtoo: Nafikiri tumeongea juu ya Wapokot, Wapokot kila wakati. Mimi kwa maoni yangu ningependelea ya kwamba, anybody who is possessing illegal fire arms should be punished. Ninasema hivi kwa sababu Serikali imependelea Wapokot wamewapatia bunduki ati wajichunge home guards wajichunge nayo, na sasa they are misusing those homeguards and they are killing us. So kwa role askari wanaandikwa askari wanandikwa ili achunge raia, sasa tukipatia raia bunduki, hiyo bunduki anatumia kuua mwenzake. Kwa hivyo ningependelea ya kwamba, wenye wako na bunduki zitolewe, hizo bunduki zitolewe. Nafikiri hiyo ni maoni yangu niko na mengi nitasema. Niko na maoni nyingine.

Jambo lingine ni wameongea juu ya wanawake na ningependelea sheria ya wanawake itunzwe to be hii yenye imekunja gender balance, sasa tupatiwe kama ruhusa kama kina mama, tukukuwe free tuna interact with others wakati unafika nyumbani unafika wakati wako sio ati ukifika mzee anakwambia mama unatoka wapi saa hii? Na unachapwa. Nafikiri ni hayo asante.

Com. Lethome: ungetaka kusema nini kuhusu kitu inaitwa domestic violence ama hii mambo ya akina mama kupigwa, violence against women or against wives utasema nini?

Albina: Ningependa kusema ya kwamba anybody mwenye anatatiza bibi yake sheria ichukuliwe anaenda kufungwa.

Com. Lethome: Wazee wamesikia hiyo. Tupate mama mwingine, njoo ujiandikishe hapa. Mrs. Clara Chebet.

Clara Chebet: Asante nachukua fursa hii kuongea juu ya waalimu. Tunaona katika upande huu wa tunaona ya kwamba waalimu wanauawa na kila mara tunasikia waalimu wanauawa, si ni hivyo? Wanauawa lakini hakuna wenye wanakunja ku-replace hawa waalimu,

Interjection Com Lethome: Chebet umesema jina yako kwa mice, umesema jina lako kwa mice, sema I-recodiwe.

Chebet: Bado sawa asante jina langu ni Clara Chebet

Com.Lethome: Ni mwalimu wewe? Endelea mwalimu sasa.

Chebet: Hee, ni mwalimu asanti, sasa nilikuwa nasema tu nachukua fursa huu kuongea juu ya waalimu, mara nyingi tunaona katika upande huu wa Ufa specifically Marakwet tunaona walimu wengi wanauawa lakini si unaona hiyo shule sasa yenye huu mwalimu alitoka kuna pengo hakuna mwenye ana replace huyo mwalimu sasa ningependekeza tu ama ningependekeza, serikali ichukue hatua kama sasa mwalimu akitoka hapa si unaona anawacha pengo kwa hiyo shule, mwalimu andikishwe, ama andikwe kwa hiyo shule yenye aendeleze hiyo kazi, sasa hiyo tu ni maoni yangu juu ya waalimu. Sorry replacing teachers where the (inaudible) were being affected, so thank you.

Com. Lethome: Mwalimu hukutwambi habari ya mishahara ya walimu na

Chebet: Hiyo ni kawaida si nimeona kama ilikuwa imeongelewa tu, wamesema waalimu waongezwe mishahara. Kama ni mimi mishahara iongezwe si unajua hiyo kazi ya mwalimu ni kazi ngumu sana, unaona hiyo kazi usiku ukitoka tu darasa, unaenda usiku unaadika, hakuna kulala. Sasa hiyo asa hiyo pengine sasa unajua kama uko na shamba lazima uadike mtu mwenye anakusaidia, hiyo mishahara kidogo haitakufanyia kazi. Sasa ningependekeza tu waalimu tu waongezewe mishahara.

Com.Lethome: Ngonja, na unajua ya kuwa wabunge wao wenyewe ndio wanajipitishia mishahara? Ungependa waendeleo hivyo kujipitishia mishahara yao wanajiamulia mishahara, waalimu nao wakitaka mishahara wanajipitishia, wengine pia wanajipitishia, ungependekeza aje?

Chebet: Ninajua hata wabunge si unajua kuna hii kazi, ubinafsi, mtu anajichagulia tu kula mishahara nono, hali hajali masilahi ya mwingine. Sasa kama ingekuwa ni mimi, hawa wabunge wawache hiyo yaani wanajisikia tu, sasa wawache huo ulaghaji na wasinyanyase waalimu.

Com.Lethome: Nani sasa aamue mishahara wao? Who should be determining the salaries of MPs?

Chebet: Sisi tuamue tu tuambiwe sisi tupatiwe nafasi ya kusema wabunge wasikule hiyo mishahara minono. Ndio sasa hiyo

Katiba ndio tuseme hata sisi raia tupatiwe hiyo nafasi tuseme wabunge wasikule tu mishahara nono.

Com. Lethome: Asanti sana mwalimu ukajiandikishe pale mwalimu, tunaendelea, Wilson Kibor Njoroge tumeambiwa ameondoka hayuko, David Yegor, David Yegor hayuko Yego huko, na Kaboyon Yano yuko ama alizungumza? Kuna Yano alizungumza hapa ni wewe, utamfuata huyu.

David Yego: *Ng'olio nyo mwore ko katiba nibo ane ne bo markweta, omwore ngo ng'oliondenyo nyo choronende koshita anende amu onyo ole nyochoech bichu, omwore kilo, shita chonyoru cha suwere en kondany'un, kobwa bik cho kitumda korotik biich che menye ariro.*

Translator: Kile kitu nasema kwa Katiba ambayo inakuja sehemu hii ya Marakwet kwa leo, ni juu ya wale ambao wanamwaga damu ya wengine, hao ni Wapokot.

Yego: *Omwoe kongoi omun okere emoni Kenya ne karam, amun emoni markweta kwa sababu motinye barabara, motinye ngo sipitali komotinye markweta, kekere kele kawalak Kenya akinee, omwoe kongoi nda kawalak Kenya tosoben koroni*

Translator: Nitashukuru sana kwa sababu naona kama Kenya imebadilika. Sisi kama Marakwet hatukuwa tumepata uhuru hatukuwa tumetengenezewa barabara, mahospitali, naonelea kwamba katika kurekebisha hii Katiba tutakuwa na uhuru wa kutengenezewa mambo haya.

Yego: *Aya ingo tar katiba ng'alechu. Ko kora kongoi kilo owal anyun kanyi markweta mochetumdoi korotik kile kitumdonu konyee cholik sosom ketumdoi markweta kirotik, keseni markwata maitin, komii bik kowole cho koalda borwekwak ko yaiky serkali chepo Kenya banyekik kobale ko cho tebe ole kowal*

Translator: Serikali ya Kenya inafikiri itabadilisha saa hii kulingana na hii Katiba, iwe kwamba hakuna mtu atabebana na hii maiti. Kama Marakwet kuwe na usalama, mtu aishi kwa amani katika nchi yake, nitashukuru kwa sababu tutakuwa na uhuru kama Wa marakwet.

Yego: *Amunee sikicham kimukon bundukinik che lochin che home guards ago mii bicho che mii sudan kilian mokite komosin, nebo samburiek ko mpuka ko lo ripe Uganda, ripei Tanzania che tinye bundukin kwa nini che choto kochome katikati mokimur nekorom markweta? Kabar markweta?*

Translator: Mbona watu walioko katikati kama Wapokot wanapewa home guards ili kwamba kutukinga na watu ambao

wanapakana nao ili wawe katikati wangepewa wale wanapakana na Uganda, Tanzania ile wajikinge na wao lakini hii ya Wapokot ni ya kuangamiza Marakwet.

Yego: *Bas ko cho che ng'alek. Ko yokere ane ko serkali chi kito keyoe serkali kou silaha che kitotoe serkali koch pokot, omwoe rani olen serkali oibe tugukwok kole chur, ogot.*

Translator: Kile kitu napendekeza kwa Serikali ni kwamba watoe silaha zote sawa ambazo wamezipatia pokot wachukue kabisa.

Yego: *Sababu komomi kir nyo kere yoche pokot ingot ak bundukinnyo chebo serkali.*

Translator: Hakuna kitu wapokot wanatumizilia kushinda hii bunduki ya Serikali.

Yego: *Bas kelecho ng'alechon ngo katiba nebo ne, owal katiba owal ngalechu bo Kenya banyinyi, komwa ra kilo soso(inaudible) serkali chebo Kenya bas mo ketrinye chon in wasiwasi saa yote*

Translator: Maneno yangu ni hayo tu kwa Katiba ya sasa, tutashukuru sana mkitenda mambo hiyo ya usalama, kuwe na usalama (inaudible) tuishi kwa usalama.

Yego: *Ko kiroke nyo mwore ane, kilen ng'alek sipitali. Kimii cho taabu bichu bo markweta. Kimii cho taabu ngo sipitali ko lo olebo maili kumi networe ko mat mokomii sipitali, sipitali nyo konyo kosorenekei markweta ko mii kapsowar ko ngonyo sipitali koyokunen serkalit hapa kwa Kenya.*

Translator: Shida nyingine ningependa kuongezea ni juu ya mahospitali. Mtu analetwa kwa bali sana anakufia tu njiani kabla ya kufikia Kapsowar. Hospitali kubwa hapa ni Kapsowar, tungependelea kuwe na hospitali ya karibu.

Yego: *Bas kongoi en ng'alecha kamwa.*

Translator: Nashukuru sana.

Com.Lethome: Yano, Kapoyan

Yano Kapoyan: *Chomwoe ane, ko ng'alek bo pokot kete tuga tugul kokete oin lang'at kilionjini ng'alek ab pokot che kete tuga tugul kou che chechwak chek kilionjini ng'alecho chek*

Translator: Naongea juu ya Wapokot, imekuwa tu ni kama siku tatu hivi imepita walichukua ng'ombe hapa Tot lakini hiyo ngo'ombe haijarudishwa mpaka saa hii, hiyo naongea juu yake.

Yano: Na ile nyingine ilikuwa DC huko Chesongoch DC yote na ma-ofisi yote sasa aliongea kama anatoa ngo'ombe.
(inaudible)

Com.Lethome: wewe unapendekeza kitu gani?

Yano: mimi napenda hiyo maneno, (iaudible)

Com.Lethome: sasa unapendekeza kitu gani

Yano: *omweo bichu.....(inaudible) mokimoche korik bii mokimoche koteben koyon chi*

Translator: Kile kitu napendekeza ni kwamba Mpokot akae kwake asikaribiane na mtu kama Mmarakwet, Mmarakwet akae kwake Mpokot akae kwake.

Yano: ndio hiyo maneno yangu mimi nataka.

Com. Lethome: Asanti sana Anthony Yego,

Anthony Yego: Kwa majina ninaitwa Anthony Yego, na ningependelea kujiunga na Katiba ya leo kwa mambo ya employment. The Government should create employment opportunities and ensure every Kenyan is employed, sababu tukiona kwa wakati huu wa Kenya wengi wamesoma lakini ukiona wengi wao wako nyumbani. Ukipata mwenye ako kazi hiyo ni bahati *nyo kilen bicho bo kutit chi ko nyo ne kole ken kotayen chito konyor kasit.* Another one is employment should be on merit. Nepotism tribalism, clanisim should be avoided, na hiyo ina tupatia shida sana. Sababu kama kuna kazi yenye watu wanataka kuajiriwa pengine kama huna mkubwa au mtu mwenye atakupeleka, hutapata kazi na ukiona wenye wako upande wa remote, ama wapi kama mtu anatoka pahali ambako hajiwezi zaidi, atakoma tu hivyo na yeye ni Mkenya. Corruption on employment should be avoided, unaambiwa toa kitu kidogo halafu upate uajiriwe. Tutapata wapi na mzee ameng'ang'ana kusomesha kijana wake, msichana wake, mpaka kidato cha nne na pengine mzee amezeeka atapata wapi pesa ya kununulia mtoto kazi tena na amesomesha?

So, nimeenda tena kwa election, ningependelea sana election ya President, MP na councilor, ningependelea zaidi watu kama hawo wasitumie pesa yani ku-campaign. Halafu watu kama wazee wa mama waweze kuchagua mtu bila kukula mali ya mtu, sababu ukiona mtu kama mzee au mama nikipatia kitu kidogo na atajiuliza kesho, wakati wa campaign atajiuliza nimekula kitu

cha mtu na lazima nimpatie na kumbe anachagua mtu mwenye sio kiongozi, na ningependelea tu pesa za campaign ikatazwe kabisa. Mtu aongee kwa mdomo wake, na achaguliwe ni hayo tu.

Com. Lethome: Asanti sana jiandikishe hapa. John Kipkech Cheserek, hayuko Jeremiah Kanda, anza na jina tafadhali I-recordiwe

John K. Cheserek: Sasa usalama ngo *bicho bonde la kerio ko mokitinye usalama ngo ane maoni kwomoche serkali chebo Kenya komomii risasin banyinya ne kekerei cho kwone kwat ne biashara. Sasa, kwa mach serkali nebo Kenya kosiman chobwone en Ethiopia, Somalia, Uganda tokokoi chu kikon risasin ngoi. Momi risasi che kioldoi.*

Translator: Sehemu hii ya Kerio kwa hivi sasa haina usalama. Risasi zinaudwa kwa hivi sasa na zinauzwa. Kwa maoni yangu ningependelea serikali iweze kuzuia risasi ambazo zinatoka Ethiopia, Somalia ili kwamba wakizuia hizi vita vitakoma.

John K. Cheserek: Ya pili ni mali ya mtu, mali ya mtu inachukuliwa hapa tuko na serikali hapa, tuko na askari lakini havuki hii mto, sijui hii Kenya iko wapi boundary? Bona iko boundary ingine hapa, askari akienda hapa tu, kufika hapa hapana hiyo ni District ingine, sasa kumbe hii ni Kenya? ningependa hawo watu askari aweke mali ya mtu mpaka mwisho wa Kenya.

Mauji vile mtu anaua mtu lazima huyo mtu anyongwe, huyo anyongwe straight kuliko pengine anaua bibi wa mtu, na huyo mtu anakaa bila kitu, huyo mtu auawe anyongwe kabisa. Halafu mashamba lazima mashamba ya hapa iwe na title deed.

Ingingine ni undungaji wa mimba, yule mtu anadunga mtoto wa mtu mimba lazima yeye amuo huyo mtoto.

Interjection Com Lethome: na akikataa?

Cheserek: Akikataa analazimishwa anafungwa, atoe fine. Siasa tupu halafu wewe utakwenda sio mbaya. Mambo ya tatu, ingine ni ya yule mtu anaoa bibi wa mtu, yule amezaa watoto wawili, tatu halafu anaimba huyo mtu afungwe alishe hawo watoto mpaka wakuwe wakubwa.

Interjection Lethome: kuna machine ina ku-record kwa hivyo usitoroke sana,

Cheserek: iko hapo kumbe hapo anasikia maneno yangu yote.

Com. Lethome: Hebu rudia hiyo ya mtu kuoa bibi wa mwingine itakuwa namna gani?

Cheserek: Mtu kuoa bibi wa mwingine, huyo mtu aletwe mpaka alishe hao watoto, kwa maana amewacha watoto wawe

mayatima, na mama yao ako hai, mtu ameo anaenda kulimia huyu shamba, anamchungia mali na huyu anataabika na watoto. Lazima huyo mtu arudishwe apeleke hao watoto awasomeshe.

Halafu wafanyi kazi, iko namna hii lazima mambo ya kuandikisha kijana aletwe mpaka kwa raia sio kusema kwa District au Nairobi, halafu mbunge anajiadikisha mtoto wa mamake, mtoto wa ndugu wake, sasa hiyo ni corruption kubwa sana. Kama hapa Marakwet mtu akienda Nairobi utaona watoto wanaenda Nairobi mwezi mzima au mwaka mzima bila kuona kitu, viatu vinaisha hakuna kazi, na mtoto ako na B+ na mbunge anaandika yule mtu yuko na D, sasa hiyo ni nini? Hiyo ni corruption. Mambo ya forest, forest lazima iwekwe security kila mahali ili raia asipite yani kuingia ndani. Sawa tu utasema yako, hiyo nimemaliza yangu.

Com. Lethome: Asanti sana John, jilandikishe hapo. Jeremiah Kanda, Jeremiah Kanda, Raphael Yano, karibu halafu ukimaliza Yano tunataka

Cheserek: kuna kitu moja nimesahau

Com.Lethome: gani hiyo.

Cheserek: Mambo ya barabara, barabara lazima iwe ya lami, kila District, kwa sababu ukitembea hapa Kenya unaona District zingine wako na lami, nyingine inakuwa District ya vumbi, halafu utume iwe haraka haraka. Ingingine kuhusu mbunge, mbunge asikuchukue mashamba kubwa kusema hii ni shamba langu acre thamanini na mimi nilimchagua yeye, mimi ninapata acre mbili na nusu, si hiyo ni corruption?

Com.Lethome: Sasa unataka apate gapi? Yule mtu yuko na mingi sana awe na ngapi?

Cheserek: Ile iko mingi iwe 10, halafu kila mmoja apate mashamba.

Raphael Yano: Asanti Commissioner kwa nafasi hii, kwa majina mimi naitwa Raphael Yano na ningependa kuchangia ya kwamba katika hali ya uongozi hapa imezoroteka sana, hasa uongozi, wa mbunge. Mbunge kwa sababu ya hii mashamba iko hapa kwetu zamani wazee wetu walikuwa na kikao cha baraza, kama kulikuweco na mambo ya mashamba wazee walikuwa wanaweza kusuruhisha kabisa bila hata maswali mengi. Lakini kwa sasa unaona viongozi hasa wanasiasa wamejiingiza kwa hayo maneno ndani sana mpaka ukienda kuangalia kikao cha DO ndiyo mwisho katika hali ya mambo ya mashamba katika sehemu hii yetu. Sasa ningependelea kwamba, mbunge awache hayo maneno ya kuingia mambo ya shamba, tuwachiie wazee, ili angalao mambo irudi kama zamani. Ingingine kuna ofisi hii inatwa ofisi ya DO, katika Serikali yetu sisi kama raia hatuoni kazi yake kabisa. Tungependelea hiyo ofisi iretrenchiwe, angalao tubaki na DC ili wa-communicate, kwa sababu ukienda kuangalia saa hii hawana kazi, kazi yao tu nikula hii kondoo ya mzee angalao apate shamba ovyo, ovyo.

Ingingine ni hii mambo ya usalama sana, tunalia hiyo kwa sababu saa hii unaona sisi tunakaa namna hii kwa sababu ukienda kuangalia sehemu za kwetu, tuko na mashamba, lakini tumekosa kulima hayo mashamba kwa sababu ya usalama, ukiinama tu namna hiyo unaona mambo ni mbaya. Kwa hivyo tunaona mambo ya usalama imalishwe kabisa katika hii bonde la, angalao Kenya mzima na yenye inachangia hayo maneno yote ni kutokua na kazi kwa vijana. Juzi kuandikwa kazi unaona mtua anaambiwa atoe elfu kadha, na unaona hiyo elfu kadha iko wapi hakuna, ndio sasa unaona vijana wanajitenga, angalao kujitafutia riziki, hata kwenda kwa upande wa town, unanyang'anywa kitu yako makusudi. So kama Commissioners chukua hiyo jawabu ya kwamba mrekebishe hiyo, Katiba ya sasa irekebishe hiyo kabisa, mtu atembe free katika Kenya.

Ya tatu, mambo ya majimbo mimi naunga sana. Kusudi angalao sisi kama watu wa bonde hili la Kerio tupate angalao kitu kidogo, kwa sababu mambo ya majimbo ikikuja kama Rift Valley, tutapata sehemu yetu. Na hiyo hata kama ni kuajili, hasa watumishi wa serikali kama askari, igawanyiwe kabisa ikuje mpaka hapa grassroot, mpaka kila location inaweza pata isiwe nyumba ingine inabembwa yote wenye hawajiwezi hawataona kitu. So hiyo ni yangu tu Commissioners.

Interjection Com. Lethome: Sasa hiyo majimbo unataka iwe katika level gani katika kiwango gani? Katika kiwango cha District, kiwango cha Province ama kiwango gani?

Yano: Province sir,

Com. Lethome: Kwa hivyo kila Province iwe na jimbo lake. Kwa mfano mimi kama si mtu wa Rift Valley na niko na property hapa Rift Valley, hata kama ni kwa mfano tuseme kuna mjaluo na ako na land yake hapa hakuna kufukuza asanti. Sasa tumpate mzee, mzee aliandika jina lingine ndio maana hatukumuita, Narok Siter, mzee Narok Siter.

Narok Silei: Mimi ni Narok Silei kwa hivyo *ng'olio ndo nomwoe roba kile nele koroni nye nde to kitoreti bicho cho lech kimukung'in. Kikitorete kimugungin mara kwanza ngete koi*

Translator: Kile kitu nasema kwa sasa ni kwamba sehemu hii hapo awali, watu ambao walikuwa hawajiwezi vilema, walikuwa wanasaidiwa

Narok: *Ndo cho korat banyinyi komotoret chi kong'et akoi ago bani ago mikestoi ago chekporotoi*

Translator: Kuna wale ambao ni vipofu lakini hawajasaidiwa mpaka sasa, na wako manyumbani, huku huku tu.

Narok: *Akitoretei tai*

Translator: na walikuwa wanasaidiwa hapo mbeleni kidogo

Interjection Com. Lethome: anapendekeza nini sasa?

Narok: Napendekeza ya kuwa, kwa nini wanacha wale ambao hawana macho, na wale wengine viwete, na zamani walikuwa wanaangalia

Com.Lethome: sasa wafanyiwe nini, unataka wafanyiwe nini?

Narok: wasaidiwe.

Com.Lethome: namna gani?

Narok: Watafutiwe, pesa ndio.

Com.Lethome: Na skuli

Narok: ya skuli, Ingingine ni wale hawana macho, pia tena wale hawana macho ndio watu wanahangaika. Kama kwa vita saa kama hii unaenda tu kugonga misituni au kugonga mawe kwa sababu hana macho ndio ningependa asaindiwe apatiwe mahali ya kuishi.

Halafu ingine kama wezi wanaiba mali ya wenyewe, mwizi kama ni upande wa Pokot ama upande wa Marakwet, kwa nini anakuja kufukuza DC, wanafukuza chief kusema kwa nini na chief hana ruhusa ambayo wanapewa yule mtu mwambie aende aue mtu, kwa nini wanafukuza? Na huo ndio uwezo wa DC, wanafukuza vijana, vijana upande wa Marakwet tangu karibu ma-chief ngapi saa hii hiyo ndiyo sababu ni mbaya sana upande huu. Mtu unaandikwa kazi saa hii, halafu kumbe wizi unatokea upande huu ama unatokea upande gani? Ndio nikuje kuita chief, chief tafuta leta hawa na chief yuko kwake, hayo ni maneno mbaya yanaonekana ni mbaya upande huu.

Interjection Com. Lethome: sasa unapendekeza namna gani?

Narok: Ninapendekeza ndio warudishiwe kazi yao.

Com.Lethome: Kama ni chief amefutwa kazi arudishiwe kazi yao, ndio kwa sababu si makosa yao Kuhusu Marakwet, Pokot umesema nini?

Narok: Ndio si makosa yao, kuhusu mambo ya marakwet na Pokot ndio serikali hata sisi tunashangaa, kwa sababu ya kushangaa ni kupewa mabunduki maelefu. Kwa hivyo hicho kitu kiko peke yake, aondoe hiyo bunduki yote kutoka kama kuna moja hata pengine wanasemana iko upande wa marakwet lakini, kama ziko aondoe yote mahali iko bunduki, halafu raia wanakaa kulingana na zamani, kwa sababu ile tabu iko hapa saa hii ni tabu kubwa sana.

Interjection Com.Lethome: Na hii tabu ilianza mwaka gani:

Narok: nafikiri sasa inaingia miaka tano saa hii ama kumi zaidi, ni kumi zamani ya wale ilikuwa zamani za usalama, usalama kwanza usalama wa kwanza ulikuwa salama, sisi tulikuwa tunakaa pamoja, mpaka sasa miaka kumi na tano ndio imezindi, miaka kumi na tano ndio imezindi saa hii, kwa mambo ya kupigana, kwa sababu tu ile hasara yetu iko saa hii, ni hasara kubwa sana. Waa angalia hata hapa saa hii, ni kubwa marakwet ni pahali mzuri sana, mahali wamejengewa mashule, upande huu, na upande huu, watu wanaishi huko manyatta ya hawa mpaka mto, na watu wanaenda hata barabara watu wanajenga mzuri, ijapokuwa tu ndio mambo ya bunduki ndio inatoka ngambo hii.

Interjection Com.Lethome: Ile bunduki ya pokot inatoka wapi?

Narok: Sijui wanatoka hiyo njia ya Kapenguria inatoka Uganda, Sultan, Ethiopia hata (inaudible) ndio wanangamiza sisi kabisa mpaka simu ya mlima saa hii, simu ya milima, tuone pengine wewe ndio unangaliwa hawa watu unafikiri wanaishi hapa, hapana ni milima. *Otertere so. ko ilanin mwoe ra babilo kitinyo kisumbuanech okoye ra ko bundukinichu aya chochani ko ne ma kinam asi ketorettech keyay kasit en koroni.*

Translator: ile kitu napendekeza ni kwamba wachukue silaha hizi ambazo ziko huku ndio tuweze kuendelea mbele.

Narok: *Amun en ko mo ba cho ye komo miten cha nyo kole chambo kok akoi akoi amomi masomo momii ki age tugul*

Translator: Wasipochukua hizi bunduki, hakutakuwa na maendeleo hatutakuwa tinalima, elimu haitaendelea, kila kitu kitasimama tu.

Narok: *Amun en koroni ko kika kitech tugun cha chang cho kikitinye en koroni*

Translator: Hapo mbeleni tulikuwa na vitu vingi tulikuwa tumejenga hata yale manyumba mnaona ilikuwa ya kitabo kidogo.

Narok: *Tokiriam ndisinik chok, tokiriam mokinik chok toki bal mbarenik chok ago momi kirinyo ki tinye nya chichi.*

Translator: Hapo mbeleni tulikuwa na ndizi, mihogo kila kitu cha kulima, na hatuna kosa lolote na huyu jirani yetu ni yeye tu ameanzisha.

Narok: *Kokomwoe kile ole, obwote ole, nyo moche kosoru banyinyi katiba nyebo ane, osoru koroni kokaramit kotese tai.*

Translator: Ile ninasema sasa ni kwamba katika hii Katiba muweze kuokoa nchi ikae kama awali, ni hayo tu.

